


Maelezo ya baadhi ya visa vya

Mathnawi ya Maulana Jalaalud-Din al-Rumi

PDF Compressor Free Version



10

Kwa lugha ya Kiswahili

PDF Compressor Free Version

Maelezo ya baadhi ya visa vya
PDF Compressor Free Version

Math'nawi Ya Mawlana Jalaalud-Din al-Rumi

Kwa Lugha Ya Kiswahili

Tarjumi imefanywa na:

Sayyid Ahmed Aqil na Hussein Hassan

Wahariri:

Prof. Ahmed Sheikh Nabhany na Ahmed Hussein Ahmed

Mchoraji picha:

Erick Mokuu

Kimepangwa katika Ngamizi na

Athman Farsi

Tarehe: Mei, 2011

PDF Compressor Free Version

PDF Compressor Free Version

Kimetangazwa na;

Idara ya Tamaduni na thakafa ya
Ubalozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran
S.L.P. 59595-00200 Nairobi

PDF Compressor Free Version

Visa vilokusanywa katika kitabu hiki ni baadhi tu ya tarjama ya tunzi zake Jalaludin Rumi. Nina imani kwamba simulizi hizi zina mafunzo kwa wasomi wote wa lugha ya kiswahili ulimwenguni.

Umashuhuri wa Jalaalud-din al-Rumi ni wenye kujieleza. Kwani yeye ni maarufu magharibi na mashariki katika nyanja zote za kielimu. Alipenda sana kutumia mashairi katika kufunza mada mbalimbali.

Sisi katika Idara ya mas'ala ya Utamaduni na thakafa ya Ubaloji wa jamhuri ya Kiislamu ya Iran, tungependa kuwashukuru wote waliohusika katika maandalizi yaliyo pelekea kuchapisha kitabu hiki. Tunawashukuru Sayyid Ahmed Aqyl na Hussein Hassan kwa juhudi zao za tarjama ya kitabu hiki kutoka kwa lugha ya Kifursi hadi ya Kiswahili. Pili, tunamshukuru Prof. Ahmad Nabhany na Ahmed Hussein Ahmed wa RISSEA-Kenya kwa kazi yao ya uhariri.

Mwisho, sitasahau mchango wa Mohammed Sadegh Amini kwa kuelezea maneno tata ya Kifursi. Mwisho kabisa, tunashukuru wafanyikazi wa idara hii kama vile Luvisia Chitala na Athman Farsi kwa kukusanya visa hivi katika kitabu hiki bila kumsahau mchoraji Erick Mokuu.

Naomba Mwenyeezi Mungu alipe juhudi ya mikono yao na visa hivi viwe ni vyenye manufaa kwa walimwengu wote.

Abbas Farmand

Mkuu wa idara ya Utamaduni na Thakafa ya Ubalozo wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, Nairobi

8 Disemba, 2011 / 12 Muharram, 1433 Hijria

PDF Compressor Free Version

Shukrani	vii
Yaliyomo	ix
Utangulizi	xi
Chemchemi Ya Mwezi	1
Kwenye Mbuga Kuu	1
Chemchemi Ya Mwezi	1
Yaliyojiri Kwenye Mbuga Kuu	3
Uvamizi Wa Ndovu	4
Mwisho Wa Kiburi Cha Mfalme Ndovu	7
Furaha Za Sungura Na Sherehe Zao	9
Baada Ya Dhiki Apata Hazina	11
Mtume Daudi aeleza siri ya mti	18
Siri ya mti wa uhai	28
Kuongea na mtu jiwe	31
Kuonana na mzee	34
Kasuku Na Mwanabiashara	37
Kasuku na mwenye duka	45
Aliye tamani kujuwa lugha za wanyama	51
Soko la Marashi	62
Mkausha ngozi katika soko la wauza marashi	62
Mshonaji Stadi na mwerevu	68
Bwana mla udongo	78
Msamiati	83
Msamiati	86

PDF Compressor Free Version

Utangulizi

*Sikiza kilio cha nai ya mwanzi cha hadithia
Kwa sababu ya kutenganishwa mbali cha shitakia
Kwenye fito ulingoni mwangu wamenivamia
Kwa maombolezo yangu wake kwa waume wanililia*

Kwa mnasaba wa kumbukumbu za Mawlana Jalaalud-Din Muhammad Balkhi, sufi na mshairi wakutoka Irani, aliyezaliwa katika karne ya saba ya Hijria. Leo Mwaka huu wa 2007 ulitambuliwa kama mwaka wa Rumi au Mawlawi. Na sisi tumechagua baadhi ya visa hivi kuwaandalia wapenzi wa utamaduni wa Jamhuri ya Kiisilamu ya Iran kwa lugha nyepesi ya Kiswahili. Usomaji wa visa hivi vya Mathnawi waweza kufungua mlango wa hazina ya thamani kwa wakubwa na wadogo.

*Ili vijavyo vizazi viweze kutia akili
Juhudi za wetu wanavyuoni wa kiasili
Zingatiani visa hivi enyi marafiki abtali
Hakika hizi nisimulizi za zetu hali*

Ni matumaini yetu kuwa hekaya hizo zitawaelimisha na kuwaliwaza wasomaji wa Kiswahili.

Ahmed Aqyl

Hussein Hassan

Mei 2011.

PDF Compressor Free Version

Chemchemi Ya Mwezi

PDF Compressor Free Version

Kwenye Mbuga Kuu

Yasimuliwa kuwa hapo zamani za kale, palikuwa na mbuga katika bonde kubwa sana. Bonde hilo lilijaa wanyama kama vile simba, chui, fisi na wengineo wengi. Katika mbuga hiyo wanyama hao walikuwa wamegawanyika katika makundi mbalimbali, wakikimbizana kwenye milima mirefu, mabonde na miteremko yake mikubwa. Walikuwa wakijistarehesha kwa vyakula na kujiburudisha kwa maji ya chemchemi yaliyokuwa yakibubujika na mito yenye kutiririka kwa wingi, katika mbuga hiyo, iliyoitwa Mbuga Kuu.


Miaka ilipita kwa raha na furaha, wanyama wa Mbuga Kuu hawakupungukiwa na chochote wala lolote. Walineemeka kwa mazuri yaliyokuwepo hadi wakajitungia nyimbo za taadhima. Hawakuwa wakijua huzuni wala mashaka katika maisha yao. Wote hao walikaa kwa raha mustarehe ila kundi la sungura tu, ndilo lililokuwa na wasiwasi, daima wa kihofia nafsi zao. Sungura hao hawakuwa na sababu ya kufurahia usiku wala mchana, kwani wao hawakuwa na pembe za kujihami wala makucha ya kujitetea, na hata hawakuwa na nguvu za kukabiliana na wanyama wakali kama vile simba na chui. Basi waliona suluhisho la tatizo hilo ni wao kuihama Mbuga Kuu na kuelekea sehemu nyingine.

Usiku mmoja baada ya kupita siku nyingi, mbali mwa macho ya samba, chui, na maadui zao hatari, sungura walikusanyika akiwemo mfalme wao, ili kufunga virago vyao na kuihajiri Mbuga Kuu. Sungura hao waliondoka kwa haraka na hima. Walisafiri masafa marefu. Walipita milima na mabonde mengi, wakitafuta sehemu itakayowafaa. Walitafuta huku na kule, mashariki na magharibi, na kila pahali, mpaka wakapata chemchemi ya maji chini ya jabali kubwa. Wote wakateremkia hapo wakapumzika.

Chemchemi Ya Mwezi

Chemchemi hiyo ilikuwa na maji safi, yaliyokuwa yakibubujika na kutiririka kutoka mlimani na kukusanyika katika dimbwi lilozungukwa na mawe pambizoni mwake. Kati ya mawe hayo yaliyozunguka dimbwi hilo, palikuwa na jiwe moja kubwa na refu, lilokaa kama kwamba

PDF Compressor Free Version



limechongwa na kupigwa msasa. Usiku ulipoingia sungura wote walikusanyika hapo karibu na dimbwi hilo, mfalme wao akapanda na kulikalia jiwe hilo kubwa. Kisha akawaita sungura na akawataka wote wawe ni wenye kuwacha shughuli zao zote ili waje wamsikize na wayazingatie atakayo waambia kwa makini. Baada ya sungura wote kuhudhuria, walilizingira dimbwi hilo na kuketi kumsikiza mfalme wao. Mfalme Sungura kwanza alimshukuru Muumba wa ulimwengu na walimwengu, kisha akawataka sungura hao waithamini neema hiyo waliyobarikiwa nayo. Aliwahimiza mbali na kula na kunywa, vilevile wajitahidi kuhifadhi chemchemi hiyo na usafi wake, na wailinde kwa sababu yao na ya vizazi vyao vijavyo.

Kabla ya Mfalme kumaliza kauli yake, ghafla pakatokea hekaheka na sauti za sungura zikavuma angani. Sungura wote waliokuwa wamekusanyika ukingoni mwa dimbwi hilo waligeuza vichwa vyao na kutazama kwa mshangao sura zao zilizokuwa zimejitokeza ndani ya maji ya lile dimbwi. Mfalme aliyekuwa juu ya wengine kwa kukaa juu ya lile jiwe kubwa, pia naye ilimbidi ashuke akaangalie kioja kilichotokea! Wote wakasogelea dimbwini na kutazama mwigu (kivuli) wa sura zao ndani ya maji hayo yaliyokuwa yametulia.

Sungura wote wakubwa kwa wadogo walisongamana na kuparagana vichwani na mabegani ili kila mmoja apate kushuhudia sura zake ndani ya maji hayo. Punde si punde, ndani ya yale maji, ilitokezea sura nyingine mpya! Na hapo ikawa ni sababu ya wao kuingiwa na hofu, wakakimbilia usalama mashimoni mwao.

Basi kama ada na desturi ya sungura panapotokea shida, wao hutoweka kwanza na kujificha, kisha baada ya hapo, wakanyemelea taratibu na polepole ili wapate kuchungulia kilichojiri. Basi hapo ndipo walipoutambua mwigu (kivuli) wa mwezi kamili ndani ya yale maji.

Mwezi ulikuwa na tabasamu, sungura walijikusanya kwa mara nyingine, hofu iliwatoka, wakajikusanya hapo kutazama sura zao tena pamoja na ile ya mwezi. Kwa furaha yao kubwa wakapendekeza chemchemi hiyo iitwe “Chemchemi ya Mwezi”.

Yaliyojiri Kwenye Mbuga Kuu

Huku nyuma kwenye Mbuga Kuu baada ya kundi la sungura kuhama, siku ngumu ziliwaingilia na ukame ulienea kote mbugani. Chemchemi na mito yote ilikauka, maua na mimea yalisambaratika na kuchanganyika na udongo wa ardhi iliyopasukapasuka. Miti ilibaki bila

majani wala matunda, na wanyama wengi waliangamia. Wanyama wengine walianza kuhama.

Lakini ndovu waliokuwa wenye nguvu na wakubwa, ndiyo kundi la mwisho kuondoka mbuga hiyo kwa kukosa budi. Ilibidi wayaache makao yao ili waziokoe nafsi zao. Mfalme wao alikuwa na umbo kubwa na uzito mkubwa, alikuwa akitoka nje kwa taklifu kufanya kazi zake.

Baada ya ugumu wa maisha kuzidi, Ndovu Mfalme alijibidiisha na wanakundi lake kutafuta maji na majani. Alipopata mitaro na maji yaliyosimama njiani, alikuwa akiingiza mkonga wake ili kuzoazoa maji atulize kiu yake. Waliendelea hivyo hadi yeye pia akawa hana tena subira. Hatimaye aliinua mkonga wake hewani akaupuliza kama tarumbeta, kwa yowe hilo la kipindi kifupi tu, ndovu wote walijumuika hapo na baada ya amri ya mfalme wao, papo hapo wakaanza mwendo wa kuondoka hapo na kutafuta makazi mengine.

Ndovu hao wenye kiu na njaa walikuwa wakitapia kila walichokuwa wanakiona njiani, na ikiwa hakikuwaridhisha walikuwa wakikisetaseta chini ya miguu yao mikubwa na mizito. Kila walipokuta miti yoyote waliizungushia mikonga kuing'oa na kuitupilia mbali. Hivi ndivyo walivyo tembea kwa siku nyingi mchana na usiku, walipitia majangwa mengi yaliyokauka hadi wakafikia ardhi ya majani na mimea.

Kwa kuwa walishukia sehemu yenye miti mingi, walianza kula maua na mimea ya nyasi ziliyofunika ardhi hiyo, walikula mpaka wakatoshaka. Kisha walikwenda kutafuta maji kwenye mlima uliokuwa karibu nao.

Uvamizi Wa Ndovu

Sungura waliokuwa kwenye maeneo ya Chemchemi ya Mwezi walifurahia sana maisha yao yenye raha tele. Punde si punde waliwaona ndovu wenye nguvu wakitokea kwa mbali, wakaingiwa hofu na wasiwasi. Kufumba na kufumbua raha na starehe zao zote ziliwaishia. Utulivu uliwaondokea katika nyoyo zao. Waliwakimbia ndovu hao na kujibanza katikati ya mawe.

Baada ya kipindi kifupi, sungura wote walijikusanya ili kufikiria suluhisho na namna ya kupata nusura. Walichungulia penyu za mawe wakiwa wamejawa hofu na wasiwasi mno. Waliwashuhudia ndovu hao jinsi walivyokuwa wakiyafuja na kuyachafua maji kwa kuyajaza matope.

*Kwa kila chemchemi ndovu kuivamia
Wanyonge waliyaona maovu daima kuwaandamia
Waoga kwa waziavu matatizo waliyakimbia*

PDF Compressor Free Version



Hali ilibaki kuwa vivyo hivyo kwa muda wa siku kumi na tatu. Kundi la ndovu lilikuwa mchana ni lenye kunywa na kuogelea, na usiku linalinda eneo la dimbwi hilo kuchunga hata tone la mwisho lisipotee na siku inayowadia maji yawe yamejaa. Ilipofika siku ya kumi na nne sungura wakiwa mbali na macho ya ndovu hao walijumuika ili kutafakari na kutafuta suluhisho kwa kushauriana na kutoa maoni. Mkongwe wao alikuwa sungura mmoja mweupe na mwenye busara, alimtamama mfalme na kumwambia: “Wahenga walisema kama hamtowedzana nguvu na maadui, basi hakuna budi kutumia hila na njama. Na kwa hivi sasa shauri ni kutafakari na kutafuta suluhisho la tatizo hili ili tuweze kutumia hila ya kuwaondoa ndovu hao, tuweze kuwa ni wenye kubaki kwenye ardhi yetu.”

Mfalme wa sungura alifurahishwa na maneno hayo yenye matumaini, lakini moyoni alikuwa na hofu, akasema: “Licha ya kuwa maneno yako yaelekea kuwa ni ya hekima, vilevile nastahili kuupongeza uwerevu wako. Lakini nahofia tusiweze kukabiliana na nguvu za ndovu hao na tushindwe kutatua tatizo hili. Naona suluhisho tulilobaki nalo, ni sisi tuiwache Chemchemi ya Mwezi mikononi mwa ndovu, tupate salama ya nafsi zetu. Lau ikiwezekana tuhamie sehemu nyengine, ambapo tutapata maisha ya faraja, mbali na maisha ya dhiki na mashaka!”

Sungura mkongwe alitafakari kidogo kisha akasema: “Ewe Mfalme mwenye busara, maneno yako ni mazuri ila tu wajua kuwa wenye hekima hawahatarishi maisha yao na wala hawaachilii ardhi yao na kuisalimisha kwa urahisi bila ya kuitetea. Lau Mfalme ataturuhusu kwanza tupange njama, basi kama itawezakana kumtoa adui, tutakuwa washindi wenye kubaki kwenye ardhi yetu. Na isipowezekana na tukashindwa basi ndipo tutakusanyana pamoja tuihame ardhi yetu hii na makao yetu.”

Sungura Mfalme alikubali, akaamrisha waandishi wamuandikie Mfalme Ndovu barua kwa hati nzuri na wanukuu kauli yake: “Ewe Mfalme Ndovu, mimi Mwezi Kamili, mfalme wa ardhi hii na chemchemi hii yangu, nakuamuru bila ya kuchelewa muondoke sehemu hii mara moja. Na lau sivyo nitayatoa macho yenu na niwadhalilisha. Basi msiwe majahili mkakosa kuyazingatia na kuyatilia maanani maneno yangu haya, mukawa ni wenye kujitumbukiza kwenye balaa. Na kama hamuamini madai haya, basi usiku huu, baada ya kiza kuingia, njooni karibu na dimbwi la chemchemi hiyo mutapata kuniona, ila tu,

musiondoke mulipoketi. Na nasisitiza kuwa musuwe ni wenye kuingiza mikonga na miili yenu kwenye dimbwi la chemchemi yangu yenye maji meupe na safi, na nikikasinka nitaamrisha hatuwa ya kuwaadhibu.”

Baada ya barua hiyo kufika kikomoni, mfalme aliweka sahihi yake na akaweka muhuri wake. Kisha akamkabidhi sungura mmoja mwenye mbio miongoni mwao ili amfikie Mfalme Ndovu mvamizi na kumsomea. Sungura mwenye mbio aliipokea barua hiyo na kwa mbio zake akapanda juu ya kilima na akanadi kwa sauti kubwa na akaanza kwa kusema “Ewe Mfalme Ndovu, mujue na mutaamali kuwa mimi ni mtumishi wa pekee wa Mwezi Kamili, mfalme wa ardhi hii.”

Maneno hayo yalimshangaza Mfalme Ndovu, hata hivyo aliwageukia ndovu wengine akasema kwa kiburi, “Maneno hayo musiyachukulie kuwa ni ya muhimu ila niporojo tu, na musitishike. Lakini kwa sababu ya kuchukuwa hadhari baadhi yenu wabaki macho mpaka asubuhi ili kuyalinda maji, na yeyote mutakaye mpata aadhibiwe na afukuzwe.” Basi waliteuwa kundi la walinzi ili wayalinde maji ya chemchemi hiyo, naye mfalme na wengineo wakaelekea matembezini mbugani.

Mwisho Wa Kiburi Cha Mfalme Ndovu

Ilisimuliwa kuwa baada ya mchana kumalizika na usiku kutanda kwenye ardhi hiyo, Mfalme Ndovu kwa machovu aliyokuwa nayo alijibwaga juu ya tifu la mchanga ambalo limejitokeza, na kufunga macho kulala. Ilitokea kuwa tifu hilo ni jumba la sisimizi, ambao walishikwa na taharuki walipokosa njia ya kutokea. Ikawalazimu kwa haraka wachimbe njia nyingine mpya iliyowachukua muda mrefu mpaka usiku wa manane! Sisimizi hao walipopata mwanya wakutoka, waliandamana kumvamia Mfalme Ndovu. Basi walimparaga mwili mzima, baadhi waliingia ndani ya mkonga wake, wengine masikioni na wengine ndani ya macho na wakamuuma muuma kwa nguvu. Ingawaje ndovu kwa maumbile yao wanausingizi mzito, lakini mwishowe uchungu wa kuumwa umwa na sisimizi hao ulifikia hisia zake na usingizi wake ukamruka, ikamlazimu apaondoke hapo alipokuwa amelala. Basi hapo kwa kuudhika bila ya kumaliza usingizi wake, aliwaondokea sisimizi hao, akajikukuta kukuta vumbi, huku akiwa amechanganyikiwa kwa muwasho wa machoni na masikioni mwake.

Alianza kukimbilia dimbwini ili kujimwagia maji na kuwakukuta hao sisimizi. Hata alipofika karibu na dimbwi, aliona walinzi wamelala usingizi, na jinsi walivyokuwa wanakoroma ilimfanya mfalme aingiwe



na hofu.

Mfalme wa ndovu alighadhabika sana kutokana na uzembe wa walenzi hao. Akawapiga vichwa vyao mateke ya na akakimbilia majini.

Akaelekea kwenda kwenye dimbwi, ghafla bila kutarajia alisikia sauti za kelele zinazopigwa na kereng'ende usiku. Akasimama kidogo na akaacha kutembea, akageuza macho kushoto na kulia, hakuona yeyote. 'Kwani naogopa nini?' Aliwaza kipekee, 'maneno ya porojo hayafai kabisa kutiliwa maanani,' kisha akaendelea na mwendo wake na kutembea kwa vishindo na kiburi. Lakini moyo ulikuwa una wasiwasi na uwoga mwingi. Akajiangalia mwili wake mkubwa na mkonga wake mrefu na kundi la ndovu waliokuwa wamelala pambizoni, akawatazama na kuwachunguza. Akajipa moyo wa kuendelea na mwendo wake, mpaka akafika kwenye dimbwi. Hata! Hapakuwepo na mtu yeyote pale. Basi akataka kuingiza kichwa chake ndani ya maji, akashtukia mwigo wa mwezi mkubwa ndani ya maji, akaanza kutetemeka na uwoga ukamzidi. Akawa anajitafutia kisababu cha kuomba msamaha na ajirudi ili aweze kupunguza uzito wa dhambi yake. Kwa bahati mbaya

kwa mkonga wake mrefu aliyadara maji ya dimbwi na akasababisha viwimbi vilivyo fanya mwigo wa mwezi kuyumbayumba. Mflame Ndovu alidhani kuwa mwezi umeghadhabishwa na matendo yake mabaya na hivi sasa atang'olewa macho yake. Ghafla mwili wake mpana ukaanza kutetemeka kwa hofu na wasiwasi kumzidi, akaona kusitasita hakufai tena, alipiga unyende na akaanza kutimuka mbio.


Usiku huo kudara maji kwa mkongawe
Mfalme kiherehere hakuhitaji mambo ayaelewe
Aliona bora ni kutoka mbio maisha ayaokowe

Ndovu waliokuwa wamelala, waliruka kutoka usingizini huku wakiwa wameshituliwa na unyende wa mfalme wao. Na kwa vile hawakupata nafasi ya kujua kilicho jiri, walimfuata mflame wao wakitimuka mbio tenge tahanani. Basi hapo ndipo walipoteara njiani ndani ya vumbi na wakatawanyika mbali na ardhi hiyo.

Furaha Za Sungura Na Sherehe Zao

Kwa vile ndovu waliamua kutoroka na kuhama ardhi hiyo, sungura wote wakubwa kwa wadogo papo hapo walitoka mashimoni wakalizingira dimbwi hilo wakasherehekea usiku mzima wakiangalia sura za mwezi, na Chemchemi ya Mwezi iliwakaribisha kwa mikono mikunjufu. Waliendelea kuwa na furaha na kuishi daima kwa raha mustarehe.

PDF Compressor Free Version



Baada Ya Dhiki Apata Hazina

PDF Compressor Free Version

*Ewe Mola muepusha kwa madhila na dhuluma
Mawi huyabadilisha kikutandikia mema
Ungapotea umtakapo hakutupi daima
Msababisha sababu milango kufungulia*

Kijana mmoja, tangu alipozaliwa na kufungua macho katika mji wa Baghdadi, aliishi katika nyumba iliyojaa neema kwa kazi aliyokuwa akiifanya baba yake mzazi. Utoto ulikuwa umeshaaga na ujana kuwasili bila ya yeye kujua huzuni wala usumbufu ni nini. Hakujuwa riziki inapatikana wapi na vipi, wala namna ya mapato yanavyotumiwa katika kula na kuvaa na haja nyenginezo. Alitumia wakati wake mwingi katika anasa na starehe nyingi. Wakati mwingine alipanda farasi wake aliyekuwa na kasi kama upepo, akienda naye matembezini milimani na kwenye mabonde, au wakati mwingine alibeba mishale na upinde kwenda kuwinda wanyama.

Mara nyengine nyakati za usiku, akiwa pamoja na marafiki zake walikuwa wakikeshwa hadi asubuhi wakila na wakinywa. Hivyo ndivyo alivyoutumia wakati wake na kufanya starehe zote, huku maisha yake yakiendelea. Siku moja babake alipouguwa, moyo wa kijana huyu ulijawa na huzuni. Mara alikuwa akiuegemea mto wa baba yake akiwa na wasiwasi kuwa baba yake siku zake za kufa zinakaribia.

Baada ya siku chache baba aliaga dunia. Kwa siku kadhaa kijana huyu alikiwa na huzuni na majonzi makubwa. Lakini yote hayo aliyasahau pale mawazo ya maisha ya anasa na starehe yalipomjia. Aliona kama kuwa baba yake hakuondoka duniani. Bali babake alimuachia urithi wa mali nyingi na utajiri mkubwa. Hayo yote aliyarithi peke yake kwani yeye alikuwa ni kijana wa pekee. Barobaro huyu aliyerithi dhahabu, fedha, majumba, farasi na wanyama wengineo. Alipata utajiri mkubwa zaidi katika mji wa Baghdadi. Kuanzia siku hiyo sifa ya utajiri wake ulienea kote mjini. Wakazi wote walimtambua.

Kijana huyu alipitisha wakati wake kwa karamu za kila siku. Hapo nyumbani kwake, kulikuwa hakwishi wageni wa kila siku waliokuja kupitisha wakati wao kwa nyimbo, ngoma na mashairi hadi usiku wa manane. Harufu za kila aina ya chakula na michuzi mbalimbali zililukia, shangwe za furaha zilimvutia kila mpita njia aliyepita karibu na nyumba yake. Kwa siku nyingi yeye alikuwa kwenye kuandalia watu vyakula na vinywaji barazani kwake na huku shamrashamra mbalimbali zikitendeka.

PDF Compressor Free Version



*Mali kumuondokea alikosa na wendani
Akawa kama bundi aliyeishi penye magofu gizani
Akamkumbuka Moliwa na kuomba kwa manani
Mimi mja wako dhaifu na sina uweza mnanisaidia*

Kwa kuwa yeye hajui jinsi ya kuchuma mali, hivyo alikosa maarifa ya kutumia mali na utajiri bila ya kufuja. Kwa mwendo wake huo aliyafuja mali yake yote aliyoyarithi kutoka kwa babake. Hakubakiwa na kitu si dhahabu au fedha, si nyumba wala wafanyikazi, si shamba wala wanyama na hata farasi wake pia hakumsaza, alisoza kila kitu. Yeye kama alivyo sifika kwa utajiri, vilevile alipofilisika alitajika kama fukara wa mji wa Baghdadi. Fakiri aliyefilisika na kubaki bila chochote kutokana na ubadhirifu wake. Marafiki na jamaa walimuhama akabaki ndani ya gofu peke yake kama bundi.

Aliunyosha mkono wake kuomba viumbe, moyo wake ulijaa majuto lakini yafaliye nini maji yaliyomwaika hayazoleki tena. Alihangaika kutafuta chakula akipatapo angalau ni tonge alishukuru, na mara nyingi alikuwa akilala njaa. Usiku alikuwa akikeshwa ili kumlilia Muumba na kumtaka amkidhie mahitaji yake. Alibeheneka na kwa unyenyekevu alimuomba Mola kwa sauti ya kuhuzunisha na kuomba magh'fira. Aliomba tena kukunjuliwa riziki yake mara nyingine huku akitubia na kuahidi ya kuwa atakuwa ni mwenye shukurani daima.

Wakazi wa Baghdadi walimsikitikia na kumuhurumia kwa ile hali aliyokuwa nayo. Huyu ndiye aliyekuwa akiandalia watu vyakula vya aina aina leo chakula chake akikipata basi huwa ni mkate uliokukutaa wakuokotwa jaani. Mwili wake ulidhoofika na hata akili ikawa haina tena utulivu, lakini hakuacha kumlingana Mola wake kwa kilio cha simanzi ambacho kila aliyekisikia kilimfanya amuhurumie na kumsikitikia.

Aliendelea kumuomba Muumba wake bila ya kukata tamaa kwa siku nyingi sana, usiku na mchana bila ya kukoma akisema "Ewe Mola kwako natubia na kwako narejea, nimeidhulumu nafsi yangu, unikataapo wewe ni nani wakunipokea? Ewe uliyejilazimisha kuwarehemu waja zako, nirehemu na mimi ni mja wako, usinitupe wala usinirudishe mkono mtupu, Ewe unayesifika kwa urahimu na ukarimu."

*Kwako nimeulekeza, uso wangu nangalia
Wakiri wangu ulimi, mimi sina tena njia
Nilighafilika ndipo ikanighuri dunia
Nepusha madhila Ewe Mwokozi nakulingana*

Siku moja baada ya maombi yake aliyafumba macho yake na kulala, hapo alijaaliwa kuona kwenye ndoto nuru kiasi ya kuwa

PDF Compressor Free Version

macho yake hayakuweza kuhimili miyale ya nuru hiyo na akasikia sauti masikioni ikisema: 'Mwenyezi Mungu amekisikia kilio chako na ametaka kukurudisha utulivu na amani. Sasa iko hazina yako ambayo imefichwa, lakini hutaipata mpaka uende ardhi ya Misri; katika maeneo ya mtaa maalumu na barabara fulani. Basi inuka na uelekee huko Misri ikiwa unaitaka hazina hiyo ili uendele na maisha yako kwa raha kama hapo awali, na uwe ni mwenye kushukuru.'

Fakiri huyo alizinduka usingizini, na kwa muda alifikiria ndoto aliyोजना. Asubuhi kukapambauka na jua kuchomoza mashariki, ndipo naye aliondoka mjini Baghdadadi kwa safari ya kuelekea Misri. Kwa tamaa na matarajio makubwa aliyokuwa nayo uzito wa safari na taabu za njiani hazikumvunja nguvu kamwe, kwani hisia zake zilimilikiwa na hazina hiyo. Aliamua kuwa atakapoipata hazina hiyo atakwenda mwenendo na njia ya mzazi wake; akijiambia moyoni kuwa 'Nitakula kiasi ya mahitaji yangu na itakayobakia nitaiweka kwa siku za usoni nitakapozeeka na vilevile niwape urithi watoto wangu nitakaojaliwa kuwa nao.'

Safari hiyo ilimchukua siku nyingi, hata hivyo alivumilia masaiibu menginjiani na taabu na mashaka yaliyomdhoofisha sana. Aliyastahamili yote hayo akiwaza kwa shauku juu ya hazina anayoitarajia ili atoke katika hali ya ukata aliyojitia kwa ujinga wake mwenyewe.

Nguvu mpya zilimuvingia mwilini alipoiona nchi ya Misri, kama kwamba alikuwa akihisi harufu ya dhahabu na fedha ya hazina hiyo iliyokuwa katika mawazo yake. Hata hivyo alitamani angalau apate mkate na maji kidogo ya kujizuia njaa, lakini alikuwa hana pesa na yuko katika nchi ya ugeni. Hivyo aliona bora avumilie na kujiliwaza kuwa hapo atakapo ipata hazina aliyoiandama ataweza kununua chakula apendacho ale ashibe. Lakini hayo yalikuwa ni mawazo tu, kwani tumbo tupu halina uvumilivu! Kwa kuona haya katika nchi ya ugenini hakuweza kuomba sadaka mchana aliona heri angoje usiku ndipo aombe ombe. Giza lilipoanza kutawala barabara na vichocho vya Misri, alikwenda kuomba omba huku jasho likimtiririka juu ya paji la uso. Alikuwa na tahayuri mno.

Wakati huo watu wa Misri walikuwa wakikimbilia majumbani wakihofo wasipatikane nje na washika doria wa Khalifa. Barabara zikawa tupu na asipate mtu yeyote wa kumnyoshea kitu. Watu wote walikuwa wametulia majumbani mwao. Kwa kuwa yeye hakuwa na pakwenda alizunguka zunguka barabarani akitarajia mema. Ghafila alimuona askari wa usiku mshika doria pekee, alimuendea na kumuomba akitarajia kupawa kitu cha kumsitiri haja. Huyu askari alimshuku kuwa yeye ni mmoja wa majambazi wanao sumbua watu hapo mjini. Hivyo basi moja kwa moja, alianza kumcharaza kwa mboko na kumlaumu kwa uchafuzi wa amani huku akimtaka ajieleze ni nini anachokifanya vichochoroni katika kiza cha usiku ule?

PDF Compressor Free Version



“Kwa nini hukutulia nyumbani kama watu wengine na kwa nini umehalifu amri ya Khalifa? Bila shaka wewe ni miongoni mwa majambazi muliowanayima watu utulivu, kuwaibia mali zao na mumemkasirisha sana Khalifa mpaka akatowa amri kuwa yeyote atakae patikana usiku vichochoroni, hata kama ni jamaa yake, tumnase, tumuadhibu na tumpeleke gerezani” askari huyu alisema.

Kipigo, adhabu aliyoipata na dhiki ya njaa, ilimfambia apige unyende na kusema: ‘Ewe mlinzi hebu nihurumie, miye ni mgeni fukara nisiyejiweza, usiendelee kunitesa! Pulika kiasi kidogo ili nipate kukuelezea yaliyonipata. Ama kuvunja kwangu sheria ni kuwa mimi ni msafiri na msafiri ni kafiri.’

Mlinzi alishangazwa na maneno hayo, alikunja nyusi na kusema: ‘Jambazi wanipandishia sauti na kutoa madai ya uongo, sasa unafanya hatia mara dufu.’ Askari alitaka kumuongeza kipigo lakini macho yake yalipokutana na macho ya mshukiwa alisita na akatingisha kichwa chake.

Alitaka mshukiwa aeleze ukweli awataje wenzake wengine ambao anashirikiana nao. La sivyo basi, machungu yote yatamuangukia yeye kwani atachukuwa hatua ambayo wezi wengine watapata funzo ili nao wasirudie au hata kufikiria kutenda uhalifu kama huo tena.

Fukara huyo askari huku akitoa kiapo kuwa yeye si jambazi bali ni mgeni kutoka Baghdadi na kaja katika nchi hii ya Misri, na ule ndio usiku wake wa kwanza. Na aliingia vichochoroni kuomba watu sitara, chakula na malazi, lakini badala yake ameuona upokeaji na ukarimu wa watu wamisri, ni kula mboko.

Haikuchukuwa muda mrefu, mlinzi aliweza kutambua kwamba huyu kweli ni mgeni aliyetoka nchi ya mbali.

“Kwa nini wewe umetoka Baghdadi mji wako na kuja kujidhalilisha katika ardhi yetu? Mbona umetembea masafa yote hayo na kuja mpaka hapa, pengine kuna rafiki au jamaa ama mtu unayemjuwa hapa?” askari alimuuliza Yule fukara.

Fukara akapata nafasi ya kujieleza akasema: “Kuna zama mimi nilikuwa tajiri niliyemiliki dhahabu, fedha na mali nyingi sana nilyoirithi kutoka kwa baba yangu. Bila kujuwa namna ya kuzichunga, zote zilikwenda na upepo na mimi mwenyewe nikawa fukara wa kuhangaika.”

“Ama kilicho nileta hapa kuna mtu niliyemuona usingizini aliyenielekeza katika ardhi yenu. Hii ilikuwa ni baada ya mimi kurejea kwa Mwenyezi Mungu na kumlalamikia usiku na mchana. Nilionyesha majuto ya dhati yangu moyoni na kumlilia yeye hadi usiku mmoja nikafahamu kwa rehema zake kuwa amenikubalia maombi yangu. Alinjia mtu usingizini akanipa ufunuo wa hazina iliyofichwa nchini Misri. Hii ndiyo sababu ya mimi kuja Misri ili nipate kuitafuta hazina hiyo na nitowe na mimi nitoke katika dhiki hii niliyonayo” fukara aliendelea kujieleza.

Mlinzi kusikia maneno hayo aliangua kichoko cha sauti iliyojaza kichocho na kuondoa kimya kilicho kuwa kimetanda wakati huo. Alipokifu kichoko chake alisema: “Ni kwa sababu ya ndoto na tamaa kubwa, uliondoka mji wako, ukavumilia dhiki na misuko suko ya njiani, ukaja hadi Misri. Ukahatarisha maisha yako kutembea katika vichocho hivi vitupu gizani, vinavyotishia hata wenyeji wenyewe. Basi usumbufu wako ni kutokana na ujinga na upumbavu, kwani hata mwehu asingeyafanya hayo. Ingawa umekuwa dhalili lakini nakuona ni mwenye heshima yako na hakika mgeni ni kuku mweupe; nusura nikushike kama mwizi na nikutupe gerezani.”

“Ewe rafiki mimi nimekuwa mwenye kuota ndoto kama hizi mara kwa mara. Ndoto yenyewe ilikuwa nzuri na yakushawishi kama hiyo yako, isipokuwa wewe alikuelezea kuwa iko Misri. Mtu aliyenijia mimi katika ndoto yangu alinihakikishia kuwa hazina kubwa iko katika mji wa Baghdadi katika gofu fulani na njia fulani na mtaa kadhaa.”

Mwana Baghdadi fakiri kusikia maneno hayo alipigwa na mshango na kuatama mdomo wazi! Maelezo haya ya huyu mlinzi yalikuwa yakiashiria mahala anapo paelewa vizuri, kwani hapo si pengine ila ni katika jumba lake liloporomoka na kuwa gofu. La kustaajibisha nikuwa huyu mlinzi aelezea habari za hapo pahala kinaganaga na hajafikapo Baghdadi mbeleni.

Mlinzi aliendelea: ‘Mimi ndoto hii nimeiyona mara kadha wa kadha lakini sikuwa kama wewe niache nyumba yangu na mji wangu nihangaike jangwani kwa tamaa yakuwa hiyo ndoto inaweza kuwa ni ya kweli.’

Kijana baada ya kusikia maneno hayo, alisahau uchungu wake na alianza kumshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu kisha akasema: ‘Lenye mwanzo lina mwisho na mkata hana kinyongo. Maumivu niliyokuwa nayo yameniondokea kwa maelezo yako haya mafupi. Sasa ukitaka kunita mjinga ama mwerevu hiyo ni hiyari yako. Nafsi yangu imezinduka kutambua niliyokadiriwa na Mola wangu, aliyenitoa katika dhiki na ghururi za kilimwengu. Mja kupata taabu na dhiki ni kheri kwake, yote yatoka kwa Muumba. Lau si kuhangaika namna hii nisengejuwa kukosa ni nini na wala mlala hoi yuhali gani.’

Siku ya pili alianza mwendo wa kuelekea Baghdadi huku akiwa nimwenye kumshukuru Muumba kwa kupata udokezo wa hazina ile. Alifukuwa ile hazina kama ilivyoenezwa kwenye ndoto ya Yule askari na akafaidi. Wakati huu alijuwa jinsi ya kuishi na kutumia mali yake kwa uwangalifu. Pia aliwahurumia mafukara na kuwasaidia.

Mtume Daudi aeleza siri ya mti

PDF Compressor Free Version

Maulana katika Mathnawi yake, amesimulia kisa cha kushangaza kilicho tokea katika zama za mtume Daudi. Kisa chenyewe kilimuhusu bwana mmoja masikini aliyekuwa na bidii ya kazi mbeleni, lakini baadae aliamua akae nyumbani kwake kuomba riziki yake bila ya kufanya kazi. Sababu ya kutenda hayo ni kuwa siku moja aliota ndoto iliyomfahamisha kuwa ataweza kupata mali na kuwa tajiri maishani mwake.

Basi yeye alikaa nyumbani kwake kipembeni na kuinua mikono kumuomba Mwenyezi Mungu. Hakika yeye aliamini ndoto yake haikuwa ni ya uongo, na hata hivyo muomba Mungu hachoki. Aliendelea kukaa na kuomba kwa sauti ya huzuni:

*Ewe Mola Ewe Muumba
Daima kwako naomba
Mjao sichoki kuomba
Nipa riziki bila ya dhiki*

Watu walimshauri asiishiriki ndoto hiyo inayokwenda kinyume na kaida za kila leo. Wengine walimnasihi kuwa hivyo anavyo fanya si sawa, na kama tujuavyo ni kuwa mtu hula nguvuze. Huyu bwana hakutaka kusikiza yote hayo, hivyo aliwaudhi watu wengi, hata wengine walimchukia na walimuona ni mtu mvivu. Alidharauliwa akafanywa jura asiyekuwa na akili. Watu walizidi kumkejeli wakimvunjia heshima wakimwambia: “Lau ungekuwa ni mtu dhaifu huna uwezo, basi tungekushika mkono na kukusaidia, lakini hatuoni haja maadamu umzima kama ndovu na nguvu unazo. Ama ndoto yako tunakuombea heri, lakini kaa ukijua mtego bila chambo haunasi. La sawa ni ukatafute riziki ya halali kwani kukaa na kusema halua halua, hakupashi kinywa utamu.”

*Waja walimcheka kwa yake maneno
Tamaa ya baidi haina mfano
Kweli bila taabu na mapambano
Mja hupata riziki pasi na dhiki?*

Mja hapati riziki pasi na dhiki
Kila haja na matakwa kubariki
Ni bidii na usulubu thabiti
Nakujaza mkono mtupu haurambwi

Siku moja alipokuwa akiendelea na uradi wake huo, ghafla kishindo kikubwa kilitokea upande wa uani mwa nyumba yake. Alishituka! na haraka alikwenda kuangalia kumetokea nini huko. Kishindo hicho cha sauti kilikuwa ni cha mlango wake kuvunjiwa! Aliuona mlango wa nyumba yake uko chini umetekuliwa kwa nguvu pamoja na bawaba zake na komeo pia. Ng'ombe aliyekata kamba na kutoroka huko atokako aliugonga mlango huo na kuung'olea mbali.

Huyo bwana alipomuona ng'ombe aliyekuwa amenona na akihema kwa uzito, amesimama hapo uwani, ametulia bila kuwa na tume yoyote ile, alitaawili kuwa maombi yake yalijibiwa hivyo basi akashukuru.

Bila ya kufikiria kuwa huyu ng'ombe ni mali ya watu, asaa amtafute mwenye ng'ombe na adai gharama za mlango wake pamoja na uharibifu uliofanywa na ng'ombe huyo; hilo halikumpitikia kutokana na tamaa kubwa aliyokuwa nayo.

Bwana huyu alichukulia kuzuka kwa ng'ombe nyumbani kwake ni kutokana na maombi yake na akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliyeniletea ng'ombe huyu nyumbani kwangu. Ni ishara kuwa ombi langu limejibiwa, naye Ananijaribu iwapo nitamshukuru ama nitamkufuru. Nami hivi sasa nitamchinja huyu ng'ombe nifurahikie ukarimu wa Mola wangu. Kisha ningojee ninayoyatarajia yote nilyomuomba kutoka kwake."

Yule maskini alimpapasa papasa ng'ombe huyo kisha akasema: "Najua nitafanya nini kwa sasa. Mwenyezi Mungu amekuleta kwangu, mimi sitokula hata kinofu kimoja cha nyama yako. Nitamshukuru Mola wangu aliyenijibu matakwa yangu nitaitoa sadaka nyama yako. Kisha nitaigawa kwa walio masikini na wasiojiweza."

Watu wa mji walishangaa walimuona mlufa huyo hohe hahe akiwa mwenye furaha na kucheka huku akiwagawia masikini na wasiojiweza nyama ya sadaka. Habari zilienea mji mzima mpaka zikamfikia mwenye ng'ombe aliyekuwa akimsaka mnyama wake. Alifika haraka hapo nyumbani kwa huyo maskini na kuanza kudai ng'ombe wake aliyechinjwa.

"Ewe! dhalimu uliyekosa mizani ya uadilifu. Waelewa kuwa ng'ombe kupotea si jambo geni hapa kwetu. Ewe! Mzoea bwerere! Ng'ombe

PDF Compressor Free Version



wangu umemchinja na kumla, utanilipa ama sivyo utakiona kilicho mtoa kanga manyoya” mwenye ng’ombe alifoka kumkemea yule maskini.

PDF Compressor Free Version
Muombaji alisema: “Riziki lilijileta kwangu, si mimi niliyetoka kuitafuta. Nilikuwa nikiomba kwa unyenyekevu na huzuni. Huyu ng’ombe alikuja mwenyewe kwangu sikuwa nimeacha mlango wazi! Basi nimemchinja nikijua ni wangu. Maombi yangu Mola ameyaitikia. Ng’ombe kupotea kweli si jambo geni, huvunja zizi kukimbia, havunji milango ya nyumba za watu na kuzingia humo ndani.”

Mwenye ng’ombe alighadhabika zaidi akamkaba mashati na kumtia nguvuni, huku akisema: “Enyi waja! Hebu amueni. Huyu bwana anadai mali yangu ati kwa dua zake ng’ombe wangu amekuwa ni wake! Nihukumieni kwa haki iwapo huyu si mwizi basi ni nani?”

Bwana muombaji, hakufikiria kuwa suala hili litafikia kuitwa mwizi, kwa ule uwepesi wake wakuamini ni riziki yake, aliweka kifua chake mbele kama ngao na kumjibu mwenye ng’ombe: “Mimi nilitaka riziki yangu ya halali, kwa njia ya sahali. Leo Mola Ameniletea ng’ombe nyumbani, sikutoka nje kumtafuta. Mbona leo naambiwa ni mwizi?!”

Suala hili lilizidi kuwa kubwa. Tangu lilipokuwa ni tete sasa limekuwa ni moto. Watu walijumuika hapo kumtetea mwenye ng’ombe na kumhimiza asirudi nyuma na tena asimuonee huruma huyo mtaka vya bure. Masikini aliyekuwa akiomba sahali ya kujipatia riziki yake, leo amejikuta katika kizaazaa dhidi ya mtu mshari mwenye nguvu kama ndovu. Mtu huyo anayedai malipo ya ng’ombe wake aliungwa mkono na watu waliojumuiika wakimtetea na kumuhimiza: “Hakika huyu anayedai ni muomba Mungu mno ni mkosa na hatujui ni dini gani anayoandama. La sawa ni mwenye ng’ombe alipwe haki yake laa sivyo mvamia vya watu apelekwe mahakamani atiwe adabu.”

Masikini alipoona kuwa mwenye ng’ombe anampeleka kwa Mtume Daudi, bwana huyo mwenye roho safi, aliamini kuwa maombi yake yamekubaliwa, na msukosuko huu bila shaka ni wingu la kupita linalo andamwa na faraja, hakuvunjika moyo kabisa. Ingawa alihuzunika kuona watu wanamkejeli, hata wale waliopokea nyama ya sadaka kutoka kwake, pia walimcheka kama wengineo.

Alitizama mbinguni akasema: “Ewe Mola, hakuna ajuaye yakini kuwa sina dhambi katika amri hii ila Wewe, na wajua nia yangu haikuwa mbaya. Nilikuelekea kwa maombi moyoni nikijua ndoto niliyoyota ni katika rehema zako ulizomtagulizia Yusufu mwana wa Yaakubu. Uliukuza moyo wangu kwa matumaini na wala kamwe sikufanya hila. ”

Kelele za watu zilikuwa juu mno hadi zikamfanya Mtume Daudi atoke nje ya nyumba yake, apate kujua ni kadhiya gani hiyo iliyowaleta

watu hao hapo kwake.

Mwenye mashtaka akasema: “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu! Ng’ombe wangu alikata kamba akatoroka mpaka kuingia nyumba ya huyu bwana asiyetaka kufanya kazi ila kungoja vya bure. Huyu bwana alimfanya ng’ombe wangu ni halali yake na akamchinja. Sasa nimefika naye kwako unitolee haki yangu kutoka kwake.”

Masikini kumuona Mtume Daudi, alipata nafasi ya kupumua. Huzuni na uzito ulimpungukia kidogo kwani njia nzima alikuwa akipigwa mateke na ngumi. Mtume Daudi alimtazama mwenye ng’ombe ambaye vitendo vyake havikumfurahisha, na aligeuka kumtazama mshtakiwa na kumuuliza: “Je, una majibu gani? Je, anayoyadai huyu ni ya kweli?”

Masikini akasema: “Ewe Mtume Daudi! Kwa miaka sabaa nilikuwa juu ya mswala nikimlingania Mola anifanyie sahali yangu riziki. Hata hivi leo nilipomaliza kuswali nilisema ‘Ewe Mwenyezi Mungu nipe riziki kwa sahali. Ewe msababisha kila sababu nifungulie tanu mlango wa riziki.’” Mara tu nilipomaliza maneno hayo, kun fayakun alizuka ng’ombe akautekua mlango wa nyumba, aliyeingia ndani na akatulia! Nilipo muona hana taharuki yoyote ile nilimsogelea na kwa nia ya kumshukuru Mola nilimchinja na nyama yake nikaitoa sadaka.”

Mtume Daudi, alimgombeza mshtakiwa huyo na kumsisitiza aseme maneno yakueleweka, yenye dalili na ushahidi tosha. Daudi alisema: “Nisikize maneno yangu, lete hoja iliyo wazi katika mzozo huu, mapato ni mavuno mjomba, mazao usiyoyapalilia hayawi ni yako! Lipa deni la mwenyewe usione vibaya, kwa salama tuyamalize haya.”

*Yasikize maneno, hoja wazi nataka
Mapato ni mavuno, hilo halina shaka
Deni utailipa, ndivyo anavyo taka
Usoyapalilia, mazao ng’o si yako*

Mwenye ng’ombe alifurahika alipo yasikia maneno hayo, kwani yalimpa matumaini kuwa atalipwa ng’ombe wake. Na waliokuwa hapo nao pia walikubaliana na hukumu hiyo. Ama masikini alimashakani, kwani masikini hata kweli akiokota huambiwa ameiba! Alimgeukia Mola akasema:

*“Ewe Mola mkarimu mjuzi wa ghaibu,
Mjao madhulumu yanikumba masaibu,
Satari ni sitiri niepue adhabu,
Kwa yako nuru mawi hupambanua mema.”*

PDF Compressor Free Version



Lau huu ndiyo mwisho wa kisa hiki, basi haingelikuwa ni kisa kibaya: ilikuwa ni kisa cha ushindi wa haki juu ya batili. Maulana Rumi tumjuavyo asingeki hadithia kisichokuwa na undani. Utandu wa haki haufidishi haki asili, na tuujuavyo umashuhuri hufanya haki ikawa batili na batili ikawa haki.

Mtume Daudi aliyekuwa ndiye kadhi wakati huo, alielewa kuwa amri hii ina siri inayotaka kujitokeza, hivyo alimshauri mwenye ng'ombe amsamehe huyo masikini, badala yake apate sitara ya yake yaliyopita!

*Msamehe masikini huyu ni bora kwako,
Muumba ni mjuzi wa siri, msitiri yako
Vumilia subiri hiyo salama yako
Hatupi wake waja sambe vyake vipenzi?*

Mwenye ng'ombe hakufurahishwa na maneno hayo, kwa hasira akainua sauti: “Kwani ni dhambi ipi hiyo kubwa niliyoitenda hata Mwenyezi Mungu aifunike na sasa ni ifidie kwa ng'ombe wangu nisidai haki yangu? Hii kwani ndiyo hukumu?”

*“Ewe bwana zima makali
Nasaha yangu ijali,
Ni rehemaze Jalali,
Haki kwima waumbuka!”*

“Muumba kwa vipenzi vyake ni mwenye uchungu,” Daudi aliendelea kusema kwa upole: “Hukumu aliyoilingania huyu masikini, imenifikia kutoka kwa Mola mjuzi wa siri zote, nakusihi kuwa na imani umsamehe huyu kwani haikuwa ni nia yake kutenda maovu.”

Mwenye ng'ombe alijitia masikitiko, na kulalama “Uadilifu wa Daudi tuujuao umekwenda wapi leo? Kupoteza ng'ombe wangu na hasara kunipata naambiwa na haki yangu pia ni itupilie mbali! Haya ni mageni kwangu, sioni wala sisikii nataka malipo yangu tena haraka.”

Watu waliyatilia nguvu maneno hayo, nao pia wataka haki itendwe, malalamishi yalipamba moto.

Mtume Daudi alitumia mbinu zote za kumtaka mwenye ng'ombe aridhike, ajisahaulie na ayafungie macho mas'ala ya ng'ombe wake. Alijaribu kutumia hekima na utaratibu ili kumueleweshwa kuwa hali sivyo jinsi anavyoifikiria. Alimtaka ayazingatie anayomtaka, angalau kwa taamuli ndogo kwa manufaa yake mwenyewe. Lakini matakwa ya Daudi yaliangukia uziwi.

PDF Compressor Free Version

Wakati Daudi alipoona kuwa maneno yake hayatiwi maanani, aligeuka akawatizama watu waliohudhuria na kuwaambia: “Sote pamoja tutaelekea nje ya mji, sehemu ambayo kuna mti mmoja pekee uliyozeeka hapaonekani athari ya maji wala uhai, hapo ndipo nitawaeleza mambo yote.”

Rohoni mwenye ng’ombe alishtuka kusikia maneno hayo. Ghafla akahisi hatari inayomkabili. Akatia akilini kuwa mazito yaja. Papo hapo aliruka kubadili msimamo wake. Lakini halaiki ya watu waliokuwa hapo hawakumpa nafasi kamwe kubadili msimamo huo.


Watu himahima walielekea kwenda penye mti huo, huku kwa pupa wakimbeba mwenye ng’ombe na mshitakiwa juu juu wakawa kama violezi juu ya mawimbi; na kuwapeleka hadi sehemu iliyotarajiwa.

Sasa katika mazingira ya mti huu mmoja palikuwa na siri iliyofupisha ulimi mrefu wa mwenye ng’ombe. Alitamani ardhi ipasuke imzike. Dhiki ya moyo ilimshukia, kiza kilimtanda, haoni njia ya kujinasua. Leo ukweli utafichuka, kumbe kupanda mchangoma kushuka ndiyo ngoma. Maovu aliyo yatenda ujanani mwake yamerudi kumzingira, kamba ya dhalimu hukatika bila salamu.

Mtume Daudi alikieleza kisa chenyewe kwa muhtasari kama ifuatavyo: “Katika siku za nyuma huyu mwenye ng’ombe, alikuwa akifanya kazi kwa mwanabiashara mmoja aliyekuwa tajiri. Siku moja walipokuwa wanarudi kutoka safari ya mbali na ndefu ya kibiashara, ambapo tajiri alipata faida kubwa. Huyu mfanyikazi alighurika kwa tamaa ya kuyamiliki yeye mali ile. Hivyo lbilisi akamshawishi na kumpambia mawazo yake mpaka akawa hawezi tena ila atimize nia yake. Usiku mmoja alipata nafasi ya kumnyemelea tajiri yake na kumuua papo hapo. Baadae alichimba shimo na kuitumbikiza maiti ya tajiri yake na kuifukia hapa chini ya mti huu.”

“Aliyakusanya mali yote aliyoyapora hapo akayaficha, na akaingia mjini akipiga mayowe na kujiliza kwa machungu ya uongo, akisema “Amkeni! Amkeni! musiketi tu, tajiri yangu huko jangwani amevamiwa na kundi la mbwa mwitu. Mke wa tajiri kupata habari hiyo alipatwa na mshtuko uliyo sababisha kifo chake. Nao wakamuacha mtoto mhanga wa pekee. Yatima huyo alileleka kwa taabu na mashaka mara kwa huyu mara kwa yule. Katika milki aliyoirithi kwa wazee wake ni hiyo nyumba anayoishi ndani yake.”

“Sasa kwa kutokuwa na ujuzi wowote wa kazi, alirejea kwa Mwenyezi Mungu amletee sababu za kupata riziki yake ya halali na amruzuku utajiri bila taabu wala mashaka. Aliomba kwa unyenyekevu mkubwa na subira nyingi akiwa na yakini kuwa Mola razaki hatamrudisha mkono



mtupu, ila wakati ukifika na sababu kuipata riziki hiyo itokee.”

“Huku nyuma huyu mfanyi kazi alipanga kuondoa tuhuma juu lake. Alikaa kwa muda mrefu kiasi cha watu kusahau. Baadae alikwenda kuzichukua zile pesa na mali zilizokuwa za yule tajiri wake na pole pole akajianzishia shughuli. Akachuma mali nyingi sana na akamiliki majumba na mashamba. Umaarufu wake ukaenea. Huu ndio ukweli wa mambo. Leo umefichuliwa kwa kisanga cha ng’ombe. Sasa imekuwa sababu ya sisi kuujua ukweli na hatuna budi kutekeleza la haki.”

Baada ya Mtume Daudi kusimulia kisa hiki, aliamua kuwa utajiri wote huo ulitokana na rasilimali ya baba ya huyu masikini muomba dua, uwe ni haki yake.

Na hivyo ndivyo siku zote haki inavyorudi kwa mwenyewe na kamba ya dhuluma, ni yenye kukatika ingawa ni ngumu.

Siri ya mti wa uhai

PDF Compressor Free Version

Hapo zamani za kale palikuwa na mfalme aliyetawala nchi iliyosifika na ardhi yenye rotuba na mazingara yaliyoshamiri. Alipokuwa akisimama kinarani mwa kasri yake alikishuhudia mandhari iliyorembesha nchi yake kwa hisia zake zote. Aliona mimea ya rangi mbalimbali iliyosambaa upeo wa jicho, na mito ya maji safi yenye kuzizima iliyokuwa ikitiririka. Kwa upande mwingine aliona ndege, na kusikia sauti zao nzurinzuri waliokuwa wakiruka ruka juu ya miti kwa furaha. Pia aliona raia wake mabarazani wakihadithia na mambo mbalimbali kwa tabasamu na furaha.

Siku moja mfalme huyo alipata habari kuhusu nchi ya Bara Hindi, iliyokuwa na jua kali mno. Hata hivyo ilikuwa na misitu mikubwa iliyoweza kuwapa kivuli kikubwa wanyama kama vile simba, ndovu, swara na wengineo. Wanyama hao walisitirika na msitu huo. Ilisemekana kwamba katika nchi hiyo kuna mti unaoweza kuwapa watu uhai wa milele. Aidha palipo na mti huo, palikuwa na kivuli nyuma ya kila mti, vivuli ambavyo vilikuja kutafuta mti wa uhai kisiri, ili vipate kula tunda lake na kupata uhai wa daima dawamu.

Mfalme alipopokea habari hizo alitetemeka tete. Alihisi kuwa kivuli cha mauti kimmkumbatia, na hakuwa tayari kutengana na nchi yake. Ghafla bin vu! Alikodoa macho na kupiga ukelele utadhani anamuona malaika wa kifo akimsogelea huku akibeba vifaa vyake. Punde si punde mfalme alizirai na kuanguka puu!

Siku kadhaa zilipita akiwa kitandani katika hali hiyo ya kukosa fahamu. Hakuna aliyejuwa kilichomkumba. Pindi tu alipopata fahamu na kuweza kufungua macho, alichokitaka ni tunda la 'mti wa uhai'.

Njiani

Asubuhi kupambazuka mwana wa mfalme shujaa aliyejiamini, alifunga safari kuelekea Bara Hindi. Alisafiri usiku na mchana, hadi kufikia joto kali la Bara Hindi. Ndipo alipumua kidogo na moyo kumtulua kwa kutambua kuwa amewasili alikokudhamiria. Alishuka juu ya farasi wake kwa furaha nyingi. Alitembea pole pole akiitaamali ile miti mikubwa na mimea ya kila aina iliyoenea hapo. Hatimaye akateremkia kwenye mto mkubwa uliokuwa ukitiririka na vipande pande vya kuni na vitawi vidogo vidogo vikiotea juu yake. Hiyo ilikuwa ishara tosha ya kuwa

upande wa juu ya mto kulikuwa na watema kuni. Aliamua kuelekea juu ili aweze kukutana na watema kuni hao, pengine wataweza kumielezea habari za mti wa uhai na namna ya kuufikia.

Basi aliharakisha kuufuata mto huo akiwa juu ya farasi wake mpaka akaona visiki na vishuke vingi na kwa mbali akaanza kusikia boboto za shoka. Ikawa kila anaposikia mpigo wa shoka moyo wake uliingia hofu. Isije ikawa mti huo unao katwa ndiyo mti wa uhai! Hata alipofika hapo kwa watema kuni; watema kuni hao walishangaa walipomuona mtu wasiyemjua. Lakini baada ya kupashana salamu, mwana mfalme aliwaelezea watema kuni sababu ya safari yake na wao walimsikiza kwa makini mpaka akamaliza. Watema kuni waliduwaa kusikia habari za mti wa uhai, waliangaliana na kuangua kicheko kisha wakamwambia: “Sisi hatujawahi kuona mti huo wala kusikia habari za mti kama huo, habari hizo ni ngano tu!”

Maneno hayo yalimvunja moyo mwana mfalme, lakini hata hivyo hakukata tamaa, aliondoka taratibu huku akiwaza “Je hizi habari za mti wa uhai upo kweli ama ni vigano kama wanavyosema watema kuni? Itanibidi hata hivyo nisikate tamaa na niwe mpana wa mawazo, macho yangu yawe wazi na nitege masikio yangu vikali.”

Alianza kutafuta ukweli kwa kupeleleza na kupekuwa kila mti alioudhania kuwa ni mti wa uhai. Hakukata tamaa kabisa, kwani aliamini ikiwa upo ataupata, na ikiwa haupo atapata ujuzi mwengine kwani bidii ya mja haipotei bure bilashi.

Kukutana na mtu mti

Siku ya pili alipanda farasi wake kuendelea na safari yake kuelekea kwenye misitu mingine huku akiwa ni mwenye kuangalia kila upande. Mara tu! Kwa mbali alimuona mtu ameketi juu ya jabali, hapo alishuka juu ya farasi wake akamfunga na kumuendea yule mtu. Alipomfikia alistaajabu kuona mwili wa mtu huyo ulikuwa na umbo kama vipande pande vya mti vyenye rangi tofauti. Na upepo wa nguvu unapompiga kipande cha gamba kinamdondoka!

Alimsogelea polepole na kwa hadhari mpaka akaketi karibu yake akamtolea salamu. Lakini mtu huyo alionekana ni mwenye huzuni na mawazo mengi, kwani hata hakumuona mwana mfalme alivyo mfikia karibu.

Mwana mfalme alitaka kujua uwezekano wa kuufikia mti wa uhai ili aweze kwenda kuchuna matunda yake kwa manufaa ya baba yake aliyemuacha akiwa mgonjwa huko kwao. Mtu mti aliposikia maneno ya kijana huyo aliangua kicheko kikubwa sana, kicheko hicho sauti yake

PDF Compressor Free Version



ilikuwa kama mfano wa mti kupuputika.

Kisha mtu huyo akasema: “Kijana angalia umbo langu limetokana na miti na unai wangu umelungamana na kila mti katika bara hili. Kila mti ulinipa kipande cha nafsi yake ili uweze kushiriki na kuhisi safari ninazo kwenda za milimani na mabondeni, bara na baharini. Kwa hivyo nina ujuzi mkubwa na habari nyingi kuhusu miti mbalimbali. Kuna miti ya tiba yenye kutibu maradhi ya ndani na nje, miti ya kukipa chakula ladha ya kupendeza, na miti inayotumiwa kubadilisha rangi ya nywele; lakini sijawahi kusikia kuhusu mti wenye kuwapa watu maisha ya milele.”

Mwana mfalme naye akasema: “Lakini mfalme wa nchi yetu amepata kusikia visa vingi kuhusu mti huo naona itakuwa hata imekuwa ni muhali kuwa habari hizo si za ukweli.”

Mtu mti akaangua kicheko kwa mara nyingine, mpaka magamba na vipande vikampuputika mwilini, kisha akasema: “Nenda milimani, kwani milima hiyo ya miaka na mikaka, imeelekeza macho yake kwenye msitu huu, inajua siri ya kila mbegu iliyostawi pengine huenda ukapata ufunguzi wa tatizo lako.”

Kuongea na mtu jiwe

Mwana mfalme alishukuru kwa shauri hilo na akaomba kuondoka. Alipomfikia farasi wake kwanza alikaa kula chakula na kunywa maji, huku akiwaza: “Sina haja ya kuvunjika moyo kwani katika msitu huu kuna maelfu ya miti, mwisho nitafaulu tu. Lisemwalo lipo!”

Mwana mfalme akampanda farasi wake na kumtimua mbio akielekea milimani. Alimuuliza kila aliyekutana naye safarini kama anajua njia ya kuufikia mti huo. Lakini hakupata jawabu muafaka.

Hata alipofika milimani, alisimama katikati mwa mteremko wa mlima, akapumzika kidogo. Alipokwisha kumpumzika aliinua sauti yake na kusema akielekea milima: “Enyi milima ya miaka na mikaka. Mumekodoa macho juu ya msitu huu na hakuna ustawi wa mti wowote musiojua. Hebu nionyeseni mti wenye kuwapa watu maisha ya milele umestawi wapi?”

Hapo kukawa kimya aspate jibu lolote. Akakata shauri apande hadi kwenye kilele cha mlima mkubwa. Basi alimfunga farasi wake hapo chini ya mlima, na akaanza kupanda kwa shida na mashaka mpaka kileleni. Hapo katika upeo wa mlima huo aliona mtu mwenye umbo la jiwe, aliyetulia tulii! Mtu huyo alikuwa akitazama na kuchunguza kila msitu na kilichokuwa ndani yake kwa macho ya uangalifu sana. Mwana mfalme baada ya kutoa salamu na kuitikiwa kwa ishara, alisogea karibu

na kuketi. Mtu Jiwe vilevile kwa ishara alimuuliza huyo mwana mfalme analolita futa kwake ni nini?

Mwana mfalme alieleza hekaya ya mti wa uhai na malengo yake ya kuutaka mti huo. Mtu Jiwe alitabasamu na kumtazama mwewe aliyekuwa akipaa angani, akasema kwa sauti; kama mpasuko wa jiwe matumboni mwa mlima: “Ni miaka mingi tangu nitulie juu ya mlima huu na mfano wa mwewe nimetega macho kwenye msitu. Hakuna mbegu iliyostawi au kuchomoza bila mimi kuwa na habari yake.” Akaongeza kusema: “Kila anaekuja huku milimani, anaketi kwa mda juu ya mawe na hapo siri yake ya moyoni anaikabidhi kwenye mawe haya magumu. Hata hivyo mimi sijaona mti kama huo wala hatuja ipata siri kama hiyo.”


Mara kivuli cha wingu kikaenea pale milimani na pole pole kikitambaa juu yake. Mtu Jiwe akaashiria: “Mimi nautizama msitu huu peke yake lakini hili wingu laolea angani ndilo lenye kunyeshea kila mti na hufika mizizini mwa mimea yote katika bara hili. Labda kwake ukiliuliza utapata kujuwa ramani ya mti huo unao utafuta.”

Mwana mfalme akateremka huku akimfikiria na kusema: “Mtu huyu ametokana na jiwe gumu lakini moyo wake ni laini kama sufi.” Basi akapanda farasi wake kulifuata wingu, lilokuwa limefika mbali na milima. Alipita katikati ya mabonde akimtoa farasi wake resi mpaka akakifikia kivuli cha wingu kilicho kuwa kimeenea pakubwa kama kwamba kilikuwa kikimsubiri.

Mwana mfalme kwa ukemi akasema: “Ewe wingu tembezi, unaepaa juu ya misitu ya bara hili na kunyeshea miti yote. Tafadhali nijulishe mti wa uhai, unaowapa watu maisha ya daima uko wapi?” Wingu likajibu: “Pulika na uzingatie, maisha yote ni kivuli, hakikai pamoja wala hakidumu. Nami situlii pahala pamoja, natembea kwingi na nanyesha pengi. Lakini sijui nitanyesha wapi na lini. Naweza kunyesha baharini ama barani, milimani ama kwenye tambarare. Ninyeshapo kwenye mimea, nachuruzika mpaka kwenye mizizi kwa lengo la kutengeneza rutuba. Basi ikiwa maisha yangu siyajui mwenyewe, nitazijuaje siri za mimea! Lakini kwa kuwa upepo ndiyo unaonipeleka utakapo, na unapepea katika maeneo makubwa kuliko yangu, na kupitia mimea yote kwa kina, huenda upepo ukawa na jawabu la suala lako.”

Mwana mfalme akafikiria na akaona hayo ni kweli. Mara kwa mara amepata kusikia minong’ono ya mimea inavyovuma kwa upepo. Upepo nao uliyashika mazungumzo hayo na ukamnong’oneza Mwana mfalme kwa kusema: “Mimi hupepea kwa miili ya mimea hata matawi, lakini sijawahi kusikia kutoka kwa matawi maneno mengine ila kupenda kupaa na kutoweka pamoja nami.”

PDF Compressor Free Version



Mwana mfalme akajibu: “Lakini wewe hupepei matawi na mchanga peke yake, wapita kwenye milango na madirisha, na unapita baina ya watu wanaopeana siri zao.”

Upepo ukamjibu yule kijana: “Matawi, miti, milango, madirisha, nguo, watu na vyote vyengine, katu sijawahi kusikia lolote kuhusu mti huo.” Upepo ukapepea tena na kusema: “Lakini namjua mtu mmoja anayejua siri zote za ulimwengu mwenye majibu ya papo hapo. Ananyumba katika msitu mmoja miti yake imekamatana kuweka sitara baina ya ardhi na mbingu. Kila nilipompitia, yeye alikuwa katika hali ya kunong’ona, basi njoo na mimi nikupeleke kwake”. Mwana mfalme alifurahi kusikia maneno hayo na akaandamana na upepo.

Kuonana na mzee

Yule kijana alimpanda farasi wake na kutimka mbio kama upepo. Alikimbia naye mpaka wakafika katikati ya msitu ambapo aliona miti iliyofungamana na kusokotana kuelekea juu hadi mbinguni. Hapo juu aliiona nyumba moja, iliyokuwa imeundwa kwa matawi yaliyosokotana. Ukumbini mwa nyumba hiyo palikuwa na mzee aliyekuwa ameketi akiwa amefumba macho, huku midomo ikicheza cheza kana kwamba anamsabihi Mola wake Muumba na kumtakasa.

Mwana mfalme kwa muda naye alikaa kimya kusubiri hadi hapo mzee mwenye nyumba atakapo mpa ruhusa ya kuongea. Kwa kipindi kirefu kuliendelea kuwa kimya bila ya mtu kuongea, ikawa ni kama dunia nzima ilikuwa imenyamaza! Hakuna sauti za ndege wala ya upepo kuvuma, bali hata pumzi zilikuwa hazisikiwi.

Kimya hiki kiliweza kuufunguwa moyo wa mwana mfalme, na kuanza kuelewa fikra na mawazo yaliyomjia bila sauti. Kwanza alidhani labda ni akili tu inamcheza shere, hapo ndipo mara mzee huyo akafumbua macho na kusema: “Sioni shere, kwani nyoyo zinapopewa nafasi ya kuzungumza hazihitaji upepo kubeba sauti za maneno yao, nyoyo zina alaka moja kwa moja zinapolingana.”

“Hapo zama hizo za kale katika tanashati za bara kulikuwa kumejaa miti ya maua yenye kupendeza na kunukia vizuri. Hapo paliishi waja wawili waliokuwa wakipendana sana. Wawili hao walizama katika ulimbwende, kila kitu walichokiona, kilikuwa kimestawi vizuri katika mazingira hayo aali! Hapakuwepo na shari wala bari ya aina yoyote ile. Maisha ya dunia hiyo yalikuwa ni kama ukurasa mpya mweupe unaongojea mchoraji hodari. Siku moja katika matembezi yao waliuona mti mmoja wa aina ya pekee, uliokuwa mkubwa mpana na mrefu. Walijaribu kuangalia mwisho wake, lakini maozi yao hayakuufikia kilele

chake kamwe kwa ukungu mwingi uliokuwa umetanda. Walijaribu kuuzunguka na vivyo hawakuutanganya. Walikaa chini ya kivuli chake kuangalia kwa maajabu mti huo. Mara puu! Tunda la mti huo liliwaangukia. Wakaliokota na baada ya kuliona kuwa linavutia na linatoa harufu ya kupendeza, walilikata vipande viwili na kila mmoja akala kipande chake. Kufumba na kufumbua, baada ya kulimeza walijikuta wameingia katika dunia nyingine mpya! Walikuta humo viumbe vingi vya aina mbalimbali. Waliona mazingira yenye rangi ya kupendeza, na kusikia sauti za furaha na za mashaka. Waliona mambo yaliyowashangaza. Mengine ya kufarihisha na mengine ya kuhuzunisha.

Hii ndiyo hali ya ulimwengu waliyoikuta, ikawa kila siku wapata kujua mambo mapya na mageni kwao. Waliona wanyama waliokuwa wamekaa kwa salama na waliokuwa katika hatari ya kuindwa na wengine. Hapo wakaelewa kuwa dunia hii ina sura mbili. Wakaelewa kuwa kuokoka kwao kunategemea kuyajua na kuyafahamu yanayotendeka na kipi chanzo chake. Hapo walizinduka na kutaka kujua zaidi chanzo cha yote haya ni nini! Masuala mengi yalichipuka na hamu ya kupata majibu yake iliwashika.

Mzee huyo alivuta pumzi kidogo na kumpa muda Mwana mfalme yazingatie hayo aliyomuhadithia. Mzee kisha akasema: “Huo mti upo kweli, nao ni ‘mti wa elimu na hekima’. Kwani mtu yeyote aliyeshiba tunda la elimu na hekima huipa kila nafsi maarifa ya Muumba wake, aliyemuumba yeye na yote haya mengine kwa ajili yake. Tukiwarudia wapenzi hawa wawili walipotaka kumjua Muumba wao ndipo na wao walipopata maisha ya milele.”

Rudi kwenu umwambie mfalme huo mti upo katika moyo wa kila mja na tunda lake ni akili. Nyinyi mumedidimia katika dhahiri ya mti huo na mukasahau maana yake ya asili.

Kula tunda moja pale usimamapo kinarani kutizama urembo wa unayo ya miliki. Utasikia mnong’ono unaouliza: “Mfalme wakweli yuwapi? Yuwapi Muumba wa yote haya? Basi utakapompata, ndipo utakapopata kwake siri ya uhai wa milele.”



Kasuku Na Mwanabiashara

PDF Compressor Free Version

“Sijui ni kwa nini nilipokuwa mdogo, nyanya yangu alipokuwa akinitolea ngano usiku kabla ngano hiyo kuisha, huchukuliwa ni usingizi?”. Babu alimwambia mjukuu wake aliyekuwa akimngoja kwa hamu ili amtolee hadithi kabla hajalala. Binti mjukuu alitabasamu na macho yakimng’ara akasema: “Usiku huu ni zamu ya kisa cha kasuku, kisa ambacho wewe mwenyewe ulisema umekipenda zaidi kushinda visa vyote.”

Babu kama kawaida alieleza kuwa kisa chenyewe ni kirefu na angependa akisimulie kesho yake. Akamtaka mjukuu wake alale. Lakini binti alinung’unika na kumwambia babu yake: “Babu! kila siku wanambia kesho! Kesho! Mimi nataka unitolee usiku wa leo. Mimi sina usingizi babu, nakuomba kwa hisani yako nitolee kisa hicho leo leo.”

Babu alipoanza kumtolea kisa hicho cha kasuku na mwanabiashara wa Ufursi, Yule binti alitabasamu na kutulia. Babu akaanza:

Hapo zamani za kale palikuwa na Mwanabiashara mmoja wakutoka nchi ya Ufursi. Alikuwa ni mtu wa safari nyingi pia akileta bidhaa kutoka Bara la Hindi. Hali kadhalika akisafirisha bidhaa za Ufursi huko Hindi. Siku moja alinuia kwenda Bara Hindi kununua vitambara aina mbalimbali, manukato, majani ya chai na hawajji.

Kwa kuwa safari hiyo inachukua miezi kadhaa, mwanabiashara baada ya kufunganya mizigo yake, aliwaaga watu wake wote mmoja baada ya mmoja. Huko Bara Hindi katika safari zake za awali aliwahi kumnunua kasuku aliyekuwa wa rangirangi na mwenye maneno ya kufurahisha. Mwanabiashara aliona hatapungukiwa na kitu akimuaga kasuku wake pia. Alipenyeza vidole vyake ndani ya tundu la huyo kasuku kumpapasa manyoa yake na kwa simanzi akasema: “Kasuku wangu mimi naenda safari nikielekea Bara Hindi kule niliko kutoa, moyo waniuma kuwa nitayakosa maneno yako ya kunifurahisha na kunichekesha. Hata hivyo ni lazima niende, lakini huenda kukawa kuna jambo unalolitamani au kitu kutoka huko kama kumbukumbu nikuletee, wasemaje?”

Kasuku alijibu: “Tafadhali usiende, usiniache!”

Mwanabiashara aliubanua mdomo wa kasuku uliomshikilia kidole kama ishara ya kumzuia asiende. Alimliwaza kasuku wake na akasema: “Nitarudi upesi, wewe sema wataka nikuletee nini?”

Kasuku alitizama mbawa zake ambazo hakuweza kuzikunjua kwa nafasi ndogo ya lile tundu alimofungiwa, akakumbuka sauti aliyoisikia

PDF Compressor Free Version



punde tu kabla haja naswa na mtego wa windaji ikimwambia: “Paa! paa! Juu juu zaidi”

PDF Compressor Free Version

Alitizana miti na mimea hje ya tundu lake na mbingu zilizoenea, macho yakamemeteka akasema: “Vyema huko uendako utaona kasuku wengi, wenye mabawa yenye rangi yakupendeza, na maneno matamu. Utakapowaona waeleze hali yangu, waambie kuwa kasuku niliye tunduni mfungwa ninawakumbuka kwa salamu, ingawa wao ni wenye kuketi juu ya matawi ya miti na kupaa angani wakiwa huru na wenye furaha. Waeleze jinsi umbali wao umenihuzunisha na sina namna ya kuwafikia na huku niliko ni ugenini, asaa huenda wakakupa maneno ya kunifurahisha na kunipumbaza.”

Mwanabiashara aliingiwa na huruma kutokana na maneno hayo mpaka chozi likamdondoka likamuanagukia kasuku juu ya bawa lake. Kwa mapenzi yake aliyokuwa nayo juu ya kasuku wake hakupenda kumuona katika hali ya huzuni, na hakuweza kumuacha huru apae aende atakako kwa sababu alipenda mazungumzo yake yaliyokuwa ni pambo ndani ya nyumba yake.

Mfanyibiashara akaanza safari yake. Njia ilikuwa ndefu yenye mabonde na milima mingi, vumbi na upepo, mvua na jua kali, mafuriko na hata theluji. Pia alikumbana na wanyama wakali. Kiongozi wa msafara aliongoza ngamia kwa taratibu akiwa anatembea. Mwanabiashara naye akiwafuata kwenye milima na mabonde. Mwendu ulikuwa mrefu na wenye kuchosha.

Mwanabiashara alijitahidi kwa kuimba nyimbo za kumpa moyo na furaha akijipa matumaini mazuri atakayoyapata huko anakokwenda. Mwishowe aliishuhudia Bara Hindi, nchi yenye anasa mambo ya kiajabu ajabu. Alisikia ati kuwa huko bara Hindi kuna miti yenye matunda yanayotokana na dhahabu asili, hodhi zenye maji ya uhai na uzima.

Katika mji aliofikia alipendezwa na mambo mengi ya hapo. Moja wapo ya mambo hayo ni miti mirefu mno yenye matawi yaliyosambaa na kuenea. Kila tawi lilikuwa na nyumba za maelfu ya ndege wa kila aina. Ndege wenye mabawa ya rangi mbalimbali, nyekundu, manjano, zambarau, kijani na samawati. Mmoja katika miti hiyo ulipambika kwa rangi za ndege hao na kunawirika. Sauti nzuri za ndege hao zilimvutia Mwanabiashara aliyependa kuzisikiliza. Katika maishani mwake hajawahi kuona mamia ya kasuku katika eneo moja kama alivyowaona katika mti huo. Ghafla akakumbuka ujumbe wa kasuku wake wa nyumbani na kuwa alimuahidi salamu zake atawafikishia swahibu zake. Basi aliinuka na kwa sauti akawaelezea kasuku hao

mtini ujumbe wa mwenzao mfungwa huko Ufursi.

Mwanabiashara alipigwa na mshangao mkubwa baada ya kuona kisanga kilicho tuatilia salamu zake alizozifikisha hapo. Kasuku kusikia salamu hizo, waliruka kwa papatiko toka tawi hadi tawi lingine na wengine waliuzunguka mti huo kama kwamba walikuwa wakitufu, huku wengine wakipiga nyende, kama kwamba wamepatikana na msukosuko mkubwa. Ghafla akamshuhudia mmoja akitetema na kukunyaa kama mgonjwa na papo hapo akaanguka chini pwa! Mwanabiashara aliyekuwa amerengwa kwa hayo alikimbilia hapo alipoanguka ndege huyo na akamuona amepindika kama maiti.

Mwanabiashara alipiga yowe na kusema: 'Ole wangu leo, kwa maneno yangu nimesababisha kifo cha mmoja wa kasuku hawa wazuri. Kwani ujumbe niliouleta ulikuwa una maana gani nyengine ambayo huyu yalimshitua mpaka akaanguka na kufa. Pengine yule kasuku wangu ni ndugu wa huyu. Ama jee huyu ana mashikamano mazuri na Yule kasuku wanguhadi kuwa ni kama roho moja katika miili miwili tofauti?' Akabaki kulaitika: 'Laiti nisengeufikisha ujumbe huu wa huzuni, na wala sikudhania kuwa utawaathiri kiasi hiki cha kumfisha mmoja wao.'

Siku zilipowadia za kurudi nyumbani, Yule mwanabiashara alirudi akiwa na dhiki ya moyo. Toka alipomuona kasuku aliyefariki kwa kumuhuzunikia mwenziwe; alijiwa na mawazo mengi ya kuwa isiwe kuna balaa iliyomkumba kasuku wake pia! Pengine kifo cha kasuku huyu ni siri ya kifo cha kasuku wake! Ama ni ishara ya mabaya yatakayonipata huko nyumbani. Mawazo hayo yalikuwa yakimjia kila usiku alipokuwa safarini akirudi. Akawa ni mwenye kupoteza usingizi wake. Alijawa na wasiwasi mpaka alipofika nyumbani.

Alipofungua mlango, macho yake moja kwa moja yalielekea kwenye tundu la kasuku. Pindi alipomuona alijawa na furaha moyoni. Alihisi kama kwamba ameutuwa mzigo mkubwa uliomlelea kwa muda. Kasuku huyo alionyesha furaha yake kwa kumliwaza kwa maneno matamu ya kumridhisha huyo mwanabiashara.

Kasuku alinyosha bawa baada ya lingine huku akiigiza kicheko na kukariri yanayosemwa. Mwanabiashara alikumbuka idadi kubwa ya kasuku aliowaona huko kwenye mti mmoja na akistaajabu kwa kusema: "Ni ajabu gani ya wewe kuonekana maeneo haya yaliyo mbali na kwenu?"

Kasuku aliyekosa utulivu na subira aliyachukulia maneno haya kuwa ni nafasi yake kuuliza alilonalo moyoni, akasema: "Je uliwaona marafiki na jamaa zangu, na je uliwapa salamu zangu na je wamenikumbuka



angalau kwa salamu?”

Kasuku alijipukusa na kusogea karibu zaidi, akakwea nyaya za tundu lake ili ayasikize majibu atakayoelezwa.

Mwanabiashara kicheko kilimuondoka, akasema: “Niliwaona na nikawapa salamu zako lakini natamani lau nisengeliwaona na nisengelizifikisha salamu zako!”

Mwanabiashara aliendelea: “Usiwe na shaka nyoyo zao ziko pamoja na wewe. Na ajabu ni kwamba mmoja wao alikosa kujimudu alipokisikia kisa chako alianza kutetemeka kisha akaanguka kutoka juu mpaka chini mchangani na papo hapo akaaga dunia.”

Hapa babu akamkabili mjukuu wake na kumwambia: Mwanabiashara angajuta majuto yake hayamfalii kitu; yazingatie sana mafunzo yaliyomo katika kisa hiki.

Kasuku kusikia maneno hayo akawa hana tena utulivu, wala hakutaka kusikia zaidi ya hapo kwani alishagundua namna ya kuganga ndwele zake. Habari hii aliyoletewa na mwanabiashara ilikuwa na ujumbe wa hekima ya kumfungua kifungoni mwake! Ingawaje mjumbe mwenyewe hakujuwa thamani ya ujumbe huo alouleta, hakufikiria kwanini kasuku wa Bara Hindi alianguka na akaaga dunia!

Ararukiwaye na nguo ni fundi wa kuzikunja. Kasuku huyo wa mwanabiashara papo hapo alipapatika na kupiga mbawa zake akazitawanya tembe alizoekewa kula. Maji aliyoekewa nayo akayamwaga. Mwanabiashara kuona hivi alihofia kasuku wake asije akajiumiza, basi akawa na hamu ya kutaka kumtuliza na kuuzima moto wa huzuni zake. Lakini ghafla kasuku alianguka chini kwenye tako la tundu akasinyaa na kutulia kimya kabisa akabaki amekukutaa kama ukuni uliokauka.

Mwanabiashara alisogea karibu zaidi, alidhania pengine huyu kasuku amezirai, alimuekea maji mengine na chakula chengine akidhani kuwa huenda akazinduka baadaye. Lakini ilikuwa haina faida ni kama kwamba kasuku alikuwa hana hisia yoyote ile.

Alitiririkwa na machozi, akalia kwa sauti: “Kasuku wangu kwanini nimekuua. Jee ni kule kukueleza kisa cha machungu na cha kuhuzunisha? Kasuku mwenye nyimbo nzuri na maneno matamu mbona leo umezima zii?!”

Mwanabiashara alishusha pumzi na kukumbuka siku zilizopita zenye furaha, siku ambazo kasuku aliigiza na kukariri kila anachokisikia, siku ambazo akipiga mbinja kwa kelele na asubuhi akimuamsha usingizini. Basi akabaki kulaitika lau asingesafiri ama asingeyasema yale aliyoyaona huko.



Kasuku hakufungua macho yake. Alivuta pumzi zake na kujikunja. Moyoni mwake alimsikitikia Mwanabiashara aliyekuwa amekaa naye kwa mapenzi huku akimpatia chakula, maji na pahala pa usalama. Ingawaje mapenzi haya yalikuwa kama pingu zilizomfungua tunduni. alikuwa humo tunduni kiasi cha ndege kusahau namna ya kupaa. Hali ilikuawa ni ile ile akiwa tunduni siku nenda siku rudi; ni kula na kulala au kuigiza sauti na kupiga nyende ili kumfarahisha Mwanabiashara huyo.

Mwanabiashara alifungua tundu akamtoa kwa upole na masikitiko akampapasa, akambusu kisha akamueka kando juu ya nyasi zilizokuwa na ubaridi kutokana na umande wa alfajiri. Baridi ilimuingia mifupani kwa mzizimo lakini kasuku hakutingishika.

Japokuwa wakati huu hakuwepo tena ndani ya tundu la nyaya za chuma bado nafsi yake ilijihisi imo kifungoni, kwa mazowea. Kweli mazowea yana taabu. Aliwaza kuwa kwa mbawa zake ataruka na kuwa huru apae aende atakapo, ajichagulie chakula atakacho, alale atakapo, aungaane na marafiki pamoja na jamii yake. Pia alihofia mambo kadhaa. Kwa mfano mashambulizi ya ndege adui, kujitafutia chakula, kupata usalama na taklifu nyenginezo. Alijipa moyo kwa kusema: 'kila ndege huruka na mbawa zake. Kuwa huru ni bora kuliko

kuwa kifungoni’.

Ghaffa bin vuu kasuku huyu alijipukusa na kujitukusa akanyoosha mbawa zake na kusema “kwaneri” akapaa juu juu kabisa mpaka juu ya tawi la mti wa hapo karibu.

Mwanabiashara hakuamini macho yake. Alijaribu kumkimbilia amnase lakini mbio zake hazikufua dafu. Hapo tena akabaki amefadhaishwa na kuduwaa. Mwanabiashara akiwa ametatizika aliinua sauti yake na akasema: “Hii ni kadhiya gani? Kifo cha ndege siku ile na huu mchezo wa leo?”

Kasuku alirukia tawi lingine na akasikia raha kwa kutumia mbawa zake. Alicheka kisha akasema: “Yule kasuku wa Bara Hindi amenionesha kuwa njia ya kujiokoa na kifungo changu ni mimi kujifanya kama nimekufa. Yeye alinielimisha kwa hekima kuwa mfugaji wangu apendae kusikia sauti na nyimbo zangu daima dawamu. Hataniacha huru ila atakapo ona kuwa nimezimika milele. Kwa ufupi neema ya sauti yangu nzuri ndiyo iliyonichongea!”

Mwanabiashara akaelewa kuwa kila mmoja wetu yumo ndani ya tundu lake amefungiwa. Kasuku huyo akapaa juu zaidi akiwa na huru wa kwenda atakapo.

Babu aliivuwa miwani yake akamwambia mjukuu wake: “Tafakari kifo cha huyo kasuku cha kujidai kilivyompa uhuru wake na kumtoa katika kifungo. Kila unalolizowea kwa kulipenda kwa hawaa linakuwa kama tundu la kifungo chako. Mjukuu aligeuza kichwa na kutabasamu: “Nafikiria sasa nimefahamu siri ya kifo cha kujifanyisha cha kasuku.”

Kasuku na mwenye duka

PDF Compressor Free Version

Hapo zamani za kale, katika mji miongoni mwa miji ya nchi na mipaka ya ardhi hii, palikuwa na soko kubwa la kupendeza. Soko lenye kuta za matofali zilizorembeshwa na vigae vya marumaru za rangi ya samawati. Vigae hivyo vilizopangwa katikati ya matofali kama vito vya pete.

Soko hili lilikuwa na maduka makubwa na madogo, msikiti na nyumba za wageni. Pia kulikuwa na sehemu za mikahawa na njia zilizokuwa chini ya sakafu za nyumba.

Janibu ya mkahawa palikuwa na baraza la wachoraji ambamo wachoraji mahiri walikusanyika. Wanabaraza hilo waliwapa kazi ya kuchora taswira na sura. Wasimulizi wa hadithi nao walihadithia visa vya aina aina. Kwa mfano, kisa cha kasuku na visa vyenginevyo.

Mwenye duka aliyekosa wateja

Mtambaji wa hikaya hii amesema kuwa: Siku moja, hapo sokoni palikuwa na mwenye duka aliyekuwa mtu wa makamu, yaani si kajana wala si mzee. Alikuwa mkarimu na mzungumzaji mzuri, mwenye tabia nzuri na sura za kupendeza. Alikuwa ni msema kweli mwenye kusimamia haki. Aliyajuwa ya halali na ya haramu. Taaban, yeye ni mzaliwa na mwenyeji wa mji huo.

Na baada ya sifa zake zote hizi, kazi yake haikumuendea vizuri. Pato lake lilikuwa dogo sana. Alijaribu usiku na mchana kutafuta mbinu za kuwavutia wateja ili kutatua tatizo hilo. Alimvunjika moyo na akawa na huzuni kwani maisha yake yalikuwa kama mzunguko wa gurudumu la ukosaji.

Siku moja alipokuwa amechoka kazini mwake, alielekea nyumbani kupumzika. Njiani, akiwa amezama katika mawazo alishuhudia kundi la watu limekusanyika. Watu hao walikuwa wamemzingira mwanabiashara mmoja wa Bara Hindi. Mwanabiashara huyo aliyekuwa na kasuku maridadi anayezungumza kama binadamu. Watu wengi walivutiwa mno kumsikiliza huyo kasuku anavyotongoa maneno yake.

Muza duka alipomuona kasuku huyo alivyowavutia watu, aliwaza: “Pengine ndege huyu ni bahati yangu. Ikiwa nitamnunua na kumueka dukani huenda akawa ni nyota yangu. Wateja watavutiwa dukani na nitapata riziki ya ziada”.

Basi akaamua kumnunua kasuku huyo kwa bei ya ghali na akamueka dukani. Kasuku huyo aliyekuwa na sauti nzuri, mbawa za rangi pendezi na maneno matamu, aliwavutia wateja wengi hapo

PDF Compressor Free Version



dukani. Wake kwa waume, wazee kwa vijana walivutiwa na kasuku huyo. Shughuli za muuza duka ziliziidi kushamiri siku baada ya siku, huku riziki yake ikiongezeka na tamaa yake ikaongezeka.

Kuanzia hapo kasuku kwa mwenye duka, ndiye aliyekuwa mshirika wake na mwenye kumpa utulivu, ndiye rafiki msaidizi wa kazi yake iliyoshamiri na kunawirika. Hadi ikafika kuwa iwapo muuza duka hayupo, kasuku alikuwa kama mlinzi wa kuchunga na hivyo alimsahilishia kazi na kumpa mwenye duka utulivu wa moyo.

Tabia ya mwenye duka ilibadilika akawa siye tena yule wa awali aliyekuwa na hulka nzuri. Badala ya kuendesha mambo kwa moyo mkunjufu na utulivu, na kufurahia maisha yake shuwari, yeye usiku na mchana aliwaza jinsi ya kuzidisha mali na kuyarundika. Aliona ugumu hata kwa chakula chake. Alianza kuwa bahili. Alijinyima kula na kunywa, na huku tamaa ilimzidi siku baada ya siku. Ubahili huo uliendelea hata hatimaye ikawa kubaniya kwake kumemuathiri kasuku pia.

Chakula cha kasuku kikawa ni cha kupimiwa. Alipewa njugu zilofanya wadudu na zisizofaa kuliwa. Kasuku usiku na mchana alikuwa dukani. Hakuwa akitolewa na kupelekwa kwenye milima na mabustani kunyoosha mbawa zake na kujipumbaza kwa kurukaruka kama hapo mwanzoni.

Siku kadhaa zilipita katika hali hii. Siku moja, siku kulikuwa na joto mno. Soko lilikuwa tupu. Halikuwa na wateja wa haja. Muuza duka aliingiwa na hamu baada ya muda mrefu aitembele sehemu ya mikahawa. Hapo mbali na kunywa kahawa ataweze kuwajulia maswahibu zake wenye hekima na marafiki wa kale, na atapata kusikiliza mambo mengine mapya yaliyotokea yakisimuliwa.

Huku nyuma kasuku aliyekuwa amefungiwa dukani, aliwatizama ndege waliokuwa wakipaa nje ya duka wakiruka ruka kutoka sehemu moja hadi nyengine. Ndege hao walitua chini chini wakifukuzana kwa furaha. Pasi na hiyari, alihisi upweke. Aliyakumbuka misitu na mabustani yaliyojaa matunda, nafaka mbalimbali, chemchemi za maji na mito yenye kutiririka iliyoko huko Bara Hindi. Aliwakumbuka jamaa na marafiki zake waliokuwa na furaha. Wenziwe walikuwa na uhuru wa kupaa angani katika mbingu za samawati, na kutua juu ya miti wakiimba kwa furaha.

Ghafla palitokea panya aliyekuwa akijitafutia chakula. Kwa bahati mbaya panya huyo alikumbana na paka. Katika hekaheka za kufukuzana kwao, kasuku alidhania pengine paka alitaka kumhujumu yeye, huko kulimshitua ikabidi apaparike ili kujiepusha kunaswa na

paka huyo. Katika piripirika hizo bawa lake moja lilipiga chupa ya mafuta ya manukato na kuiangusha chini ikavunjika. Panya alikimbilia shimoni mwake na paka akajitafutia njia yake akaenda zake.

Kasuku alituwa kipembeni akiwa na hofu na wasiwasi huku akitizama chupa iliyovunjika na mafuta yaliyo mwagika. Baada ya muda wa saa hivi mwenye duka mbahili aliingia dukani akitabasamu akionyesha furaha moyoni. Mara jicho lake likaangukia chupa iliyovunjika na mafuta yaliyomwagika. Alihuzunika na ghafula dunia ikajaa giza kwa mtazamo wake wa hamaki. Kwa hasira aliyokuwa nayo uso wake ulipiga wekundu na macho yake yakawaka moto kwa damu kumpanda. Papo hapo alisahau wema wote wa kasuku na moja kwa moja akamlaumu kwa hasara aliyomtia. Alimuadhibu kwa kumfuchua shungi lake na manyoa huku akimsemeza ‘...baada ya mimi kukupa chakula cha bure na pahali pa usalama hii ndiyo shukurani yako leo?’

Kasuku alikaa kama aliyevuliwa nguo na aliyenyolewa upara. Alihuzunishwa na dhuluma aliyotendewa na mwenye duka aliyekosa huruma na moyo wa imani. Moyo wa kasuku uliingia uchungu. Hapo alibaki kimya. Kuanzia wakati huo, hakutamka tena, hakuwakaribisha wanunuzi, hakuwambia nyimbo za kuvutia.

Baada ya kipindi kifupi hasira kumuondokea mwenye duka ndipo alijirudi na akayazingatia aliyoyatenda akajinunguniza: “Ewe unayetoa bila kupewa! Ni yapi haya niliyoyafanya mimi na ni dhuluma gani hii niliyomtendea kiumbe huyu; hayawani asiyekuwa na hatia?”

Alijuta sana na kujilaumu akawa sasa anamsairi kasuku na kumbembeleza ili pengine kwa mara nyingine atafungua kinywa chake na aufurahishe moyo wake ulioudhika. Lakini kasuku hakuufunguwa tena mdomo wake kamwe na hakuutuliza moyo wa mwenye duka aliyejuta majuto ya Firauni.

Majuto ni mjukuu huja kinyume. Siku nyingi zilipita baada ya tukio hilo. Mwenye duka alibaki katika majuto na masikitiko. Mwenye duka alikosa utulivu na hakuwa na raha kwa kumuona kasuku wake amebaki kimya kama aliyekatwa ulimi.

Haukupita muda mfrefu, mwenye duka alijawa na hofu alipoona dalili ya kuzorota kwa pato lake na maisha ya ukosaji yanambishia hodi mlangoni. Alishuhudia tena upungufu wa riziki na kutonawiri kwa biashara yake akiama ulimi. Alijivuta nyele na ndevu na kujilaumu kuwa: “Punda mimi nileyekosa fadhila, niliyelipa fadhila kwa mateke. Ni guo gani hili la ujahili nililojivika! Ole wangu kwa moto niliojiwashia mwenyewe na kuyachoma mavuno yangu yote kwa kijichupa kidogo cha mafuta tu! Laiti ningelimeza hasira zangu. Kweli hasira hasara. Hivi



kwa mikono yangu nimejichimbia shimo la ukosaji na kujitumbukiza humo.”

Mwenye duka alijaribu kila mbinu na kuweka nadhiri nyingi ili ulimi wa kasuku ufunguke tena. Lakini kinywa cha kasuku kilibaki kimefungwa na hivyo wateja hawakuwa ni wenye kuvutiwa tena kwa mfanyi biashara huyo.

Hata siku moja pakatokea mtawa hapo dukani aliyekuwa na kidazi. Kasuku alipomuona tu alikumbuka hali yake ya kuteswa mpaka akawa na kipara. Hakuweza kustahamili akamuelekea mtawa akasema: “Ee kweli kilichompata ngwena na kiboko kimempata! Mimi nimekuwa kipara kwa kuvunja chupa ya mafuta na wewe mwenzangu nakuona na kipara kama changu. Je! Ulikumbwa na nini hata ukavunja chupa ya mafuta?”

Masikini kasuku alidhani kuwa yeyote mwenye upara alivunja chupa ya mafuta na kupata kuadhibiwa na tajiri wake!

Mtawa alistaajabishwa na maneno hayo akamtizama mwenye duka kwa mshangao, aliyeruka kwa furaha kuisikia tena sauti nzuri ya kasuku wake kuzungumza. Alicheka na kumuelezea huyo mtawa

kisa cha maneno hayo. Mtawa naye pia alianza kucheka pamoja na mwenye duka mpaka machozi yakawatoka.

Mwenye duka aliyekuwa nakujitamalaki kwa furaha alianza kucheza na kuimba. Alitaraji kuwa kwa mara nyengine ndege wa baraka amemfikia na asubuhi ya mali imepambazuka na giza la bahati mbaya limemuondokea. Kwa furaha yake alikosa hisia na akadhani kuwa sasa kasuku ameshatopoka na yaliyopita si ndwele. Hakutanabahi kuwa manyoa ya kusuku yalikuwa yamemea tena na mbawa zake zilikuwa tayari kumpeperusha atakapo.

Kasuku naye alizama kwenye mawazo mengine kabisa. Alikumbuka uchungu wa kuadhibiwa kwa kung'olewa manyoya yake mazuri na aliwakumbuka rafiki zake wa kale wanaoruka na kupaa angani watakavyo. Ilimpitikia kuwa kilichoniuma jana leo hakinitambai. Alilinganisha huria ya maisha yake zamani akiwa na marafiki zake akipaa nao angani na kutua na yale ya sasa ya kifungoni kumfaidisah mwenye duka ilihali yeye anaumia ndani kwa ndani.

Siku ya pili mwenye duka alipofungua mlango wa duka, kasuku alizikunjua mbawa zake bila ya kusema lolote. Alipiga mabawa na kupaa akielekea vichakani kukutana na wenziwe. Wote wakawa huru na kuishi kwa furaha. Alimuacha mwenye duka na tamaa yake nyingi amezubaa.

Aliye tamani kujuwa lugha za wanyama

PDF Compressor Free Version



Hapo katika zama za Nabi Musa palikuwa na tajiri mmoja aliyekuwa na kila kinacho hitajika katika maisha yake. Nyumba yake yenye nafasi na ya kupendeza lilikuwa katika shamba kubwa. Shamba lenyewe lilikuwa na mimea mbalimbali, na bustani la matunda ya kila aina. Alikuwa na wanyama kama vile farasi, punda, kuku na mifugo mingine mingi, pamoja na mtumwa muaminifu, aliyekuwa mshupavu na hodari, akimfanyia kazi zake zote.

Siku moja iliyokuwa shuwari, jua liliangaza na miyale yake ilienea na kumemeta katika mazingara hayo. Upepo mwanana ulikuwa ukipiga polepole, na kumpepea tajiri huyo aliyekuwa amekaa na kuburudishwa na mandhari ya shamba lake pamoja na mkewe. Hapo mawazo yalimjia na akakumbuka hamu yake kubwa tokea utotoni ya kutaka kujua lugha za wanyama. Hamu hii ilijitokeza tena, huku akiwa amejinyosha chali juu ya tandiko kichwa juu ya mto na guu moja juu ya lingine, na kwa sauti akasema: “Ewe Mola, laiti ungelinijaalia kuzielewa lugha za wanyama ningelifurahi sana na ningeliketi na kuyasikiliza mazungumzo yao ili nipate kufaidika.”

Mkewe aliyekuwa akidondoa zabibu moja moja akizila, aliinuka akamuuliza: “Ewe mume wangu, imekuwaje tena mbona waongea peke yako, kuna nini?”

Mume akajibu: “La, sijasema kitu, nilikuwa nawaza tu!”

Mke kwa upole akamuuliza: “Ulikuwa wawaza nini?”

Mume alitaka kuyaepuka mazungumzo hayo, lakini kwa kukosa budi na kuchelea utiriri wa mkewe, alimuelezea kisha akasema: “Hayo yalikuwa ni matamanio tu.”

Mke akasema “Mungu aunusuru ulimi wangu, kwanini wataka kujua lugha za wanyama, ama wataka kuingilia kazi isiyokuwa yako, na mambo yasiyokuhusu?”

Mume kwa mkato akajibu, “Niwache vivyo hivyo, na tusiyazungumze tena haya.”

Yule bwana aliinuka na kutembea shambani kuhakikisha kama mifugo yote imesharudi zizini salama na wamepata maji ya kutosha jioni ile. Mke alishangazwa kumuona mumewe amekatisha mazungumzo hayo kwa kujishughulisha na mambo yanayo simamiwa na mtumwa wake hapo shambani.

Usiku mmoja, tajiri huyo alikosa usingizi na kuanza kunong’ona pekee yake: “Ewe Mola niitika hili ombi langu, angalau ni mara moja tu uniwezeshe kujuua lugha za wanyaama. Kwa nini hunipi nikuombalo?”

Kama kawaida alfajiri ilipofika, jogoo ni wa kwanza kupiga mabawa yake na kuwika. Mbwa alifungua macho kivivu akaenda mwayo akarudi

kulala, akilipuuza kero la jogoo aliyekuwa akirukaruka huku na kule.

Tajiri baada ya kuamka na kumaliza ada zake za nyumbani aliwapitia mifugo yake kuhakikisha kuwa kila kitu kipo sawa. Aliwaona ng'ombe waliokuwa tayari kukamwa, mbuzi waliokuwa wakisukumana kukimbilia malishoni na mbwa aliyekuwa akimwangualia tajiri yake kwa macho ya masikitiko.

Tajiri alimtizama yule mbwa na kushangaa: "Eh! Mbwa mbona wanitizama hivyo, ama pengine Mola amenikubalia ombi langu!"

Alisogea karibu na kumuuliza: "Ewe mbwa mtiifu una nini? Je wahisi njaa ama ni ugonjwa?" Mbwa alibweka mara moja na kuondokea kando. Tajiri kwa unyonge na kusononeka alilaitika kwa kutojuwa lugha za wanyama.

Aliinua kichwa chake na kuangualia mbinguni kwa masikitiko akasema: "Ewe Mola, kwa nini hunipi uweza ni kafahamu lugha za wanyama?"

Mkewe aliyekuwa ameyasikia hayo, alishangazwa na kwa huzuni akamuuliza: "Je! fikra yako ya kuchekesha imekuja kichwani? Tamanio lako hili ni kama kutaka Mola akupe mbawa uweze kupaa angani kama kozi." Mkewe alijaribu kumkanya na matakwa hayo na kumtaka asijisumbue kwa lisilokuwa la lazima. Hatimaye bibi alimshauri mumewe aende kwa Nabi Musa apate kumuombea kwa Mwenyezi Mungu, huenda akapata kutatukiwa na masaibu yake hayo. "Sina shaka yeye atakuwa ni mwenye kukuombea. Pia kwa nasaha zake nzuri, ataweza kuyaondoa mawazo haya yasiyofaa kichwani mwako."

Fikiria hii ilimuafiki tajiri, kwani hakika Musa ni Mtume mtukufu anayependwa na Mwenyezi Mungu. Huenda akayajibu maombi yake. Leo hii nitakwenda nikamueleze tamanio langu!"

Tajiri aliharakisha kuvaa nguo zake na viatu ili atoke na kuelekea kwa Nabii Musa.

Alipofika kwa Mtume Musa, alitoa salamu kasha alikaribishwa vizuri. Naye kwa pupa akaeleza haja yake akisema: "Ewe Mtume mtukufu, ningelipenda uniombe Mola wako anipe uweza wa kujua lugha za wanyama. Hili litanisaidia kuboresha maisha yao na litanitilia nguvu imani yangu ya dini na kunisaidia kuitakasa roho yangu mbele za Mwenyezi Mungu."

Musa alikifunga kitabu kilichokuwa mikononi mwake, kisha akasimama kuyatafakari aliyoyaskia kutoka kwa mgeni aliyemjia nyumbani. Tajiri kwa sauti yakutetemeka aliendelea kusema: "Nina tamaa kuwa lugha za wanyama yaweza kuyafumbua macho yangu na kuniwezesha kutambua ulimwengu mpya ili niweze kupata utulivu zaidi

moyoni, juu ya Mwenyezi Mungu.”

Musa akamwambia: “Ewe ndugu yangu, nenda na uyaache matafahio haya kwa maana hayana faida. Ama utulivu na imani ni mambo yanaowezekana bila ya ilimu hiyo unayoitaka na mafunzo ya Mwenyezi Mungu yamekufikia kwa lugha unayoifahamu.”

Tajiri alimtizama Musa kwa mshangao na kwa kusesitiza akaendelea kusema: “Ewe Mtume mimi sitapata utulivu abadani. Fikra hii imenishughulisha mawazo yangu kila kukicha kutoka utotoni na sitatosheka ela uniombe nilitakalo!”

Musa aliketi na kufungua kitabu chake, kisha akasoma misitari fulani. Midomo yake ilikuwa inashughulika, lakini tajiri alikuwa hasikii chochote. Ghafla macho ya Musa yakajawa na mwangaza. Yeye alikuwa akizungumza na Mwenyezi Mungu akisema: “Ewe Mola, shetani anaichezea roho ya huyu kijana, aliye mwepesi wa kuhadaika. Lau nitamtekelezea matakwa yake, itakuwa ni kwa madhara yake. Na Lau sitamkubalia, imani yake itapatwa na dosari! Nifanyeje? Nipe jibu!”

Mwenyezi Mungu alimjibu: “Ewe Musa, mfunze kwa ukarimu wetu hatukatai kuyajibu maombi ya waja.”

Musa aliinua kichwa akamtizama na akasema: “Ewe kijana, nakufunza lugha za wanyama wawili tu! Mbwa na jogoo pekee. Basi angalia utakavyo itumia na ujihofie mbele za Mwenyezi Mungu!”

Tajiri hakutosheka na hayo majibu. Alijaribu kumuhimiza na kumbembeleza mno Musa amfunze zaidi ya lugha mbili hizo! Ningetaka kujuwa lugha za hawa wanyama wengine! Nataka unifunze lugha za punda, farasi na mbuzi pia!” tajiri alisisitiza

Musa hakumkubalia hayo abadani. Hata hivyo tajiri alifurahi na akakimbilia nyumbani haraka haraka. Akamuuliza mkewe kwa pupa na hamu kubwa, “Wawapi hawa jogoo na mbwa wetu?”

Mke alitabasamu na kwa utani akajibu: “Mbwa na jogoo wetu wameshalala. Masikini walikusubiri ili uweze kutoa upweke wao kwa maneno yako matamu. Yumkini wewe ulichelewa na usingizi uliwashinda nguvu.” Mke aliendelea na kuuliza: “Sasa nieleze natija ya mkutano wako na Mtume Musa. Je! Alikuombea ili urudi katika akili zako timamu ama vipi?”

Tajiri kwa sauti ya juu: “Ewe mke wangu nililokuwa nikilitaka nimelipata. Tamanio hili langu tangu utotoni, leo limetimia! Musa alinifunza lugha ya mbwa na jogoo.”

Siku ya pili alirauka na kumuuliza mtumwa wake: “Ewe Ghulamu uko wapi, je chakula tayari? Fanya haraka upesi.”

Ghulamu aliitika: “Naam chakula kiko tayari Bwana wangu!”

Alikuja kutoka jikoni akiwa amebeba sinia kubwa la shaba, iliyokuwa na visahani vya tende, asali, jubini na siagi, jagi la maziwa, mikate na matunda mengine.

Tajiri aliwatizama jogoo na mbwa kisha akawaza hawa kuzungumza ili niwasikie itabidi mbingu ishuke ardhini!”

Alipomaliza kunywa chai alirusha chenga na vipande vya mikate uwani. Kawaida kuwa ndege na kuku huja kula.

Jogoo aliyekuwa karibu alizikimbilia haraka haraka huku mbwa akimwalia jogoo anavyoipapua hiyo mikate. Tajiri alikuwa akiwazia kazi za kupanga kwa siku ile, mara tu akasikia kauli ya mbwa: “Ewe kafa mkubwa wafundira chenga na mikate pia kwa uroho kama kwamba utanyan’ganywa! Lau utaniachia mimi hiyo mikate utapungukiwa na nini?”

Papo hapo akamsikia jogoo akijibu: “Sili mali yako nala ya meza ya tajiri wangu. Kwa nini nikuachie mkate kwani mimi sifai kula?!”

Tajiri alitabasamu na kwa shauku aliyokuwa nayo, alisogea karibu kwa upole akaketi na kuwatizama kwa mshangao.

Mbwa alibweka: “Wewe waweza kula mbegu, matawi ya mboga, majani na wadudu pia. Lakini mimi siwezi, basi hata kipande hiki cha mkate ningejishikiza nacho kwa muda, hutaki kuniachia kwa uroho wako!”

Jogoo kwa madaha aliwika: “Wewe tulia huko kando, hivi karibuni Mungu atakupua kizuri zaidi ya mikate hii.” Mbwa aliinua kichwa akauliza kwa mshangao: “Ati umesema nini?”

Tajiri aliinua nyusi zake na akatega sikio kusikiliza zaidi.

Jogoo akasema: “Kesho farasi wa tajiri atafariki na mzoga wa farasi kwenu nyinyi mbwa ndiyo chakula bora zaidi kisichokuwa na mfano. Utabaki wewe peke yako na bongwe la mzoga mtamu kweli!”

Tajiri aliinuka kwa mshangao: “Ati farasi wangu, farasi wangu mrembo atafariki! Hii itakuwa ni hasara kubwa kwangu mimi!”

Alikimbilia haraka kwa mke wake na kumuelezea juu ya mazungumzo ya jogoo na mbwa. Mke alishangaa akawa hana la kusema. Alidhani pengine mumewe ameanza kuwa mwehu. Tajiri aliharakisha kabla jua kuzuka zaidi alimuongoza farasi wake kuelekea sokoni. Hata hivyo aliona uzito kuyakubali aliyoyasikia, kwani huyu farasi anaonekana mzima wala hana ila ya aina yoyote ya kuashiria kifo chake! Alimpapasa farasi wake na kumbusubusu huku akiwaza “Laiti ningelielewa lugha yako pia. Mwili wako wote ni mzima. Sijui ni kwa sababu gani kuwa kesho kwa maneno ya jogoo wewe utakuwa ni mwenye kufa!”

Alipofika naye sokoni alimuza kwa bei ya juu kabisa. Kwa udhahiri

PDF Compressor Free Version



farasi huyo alionekana kuwa ni mzima na mwenye nguvu.

Tajiri alifurahika sana akaona kuwa amepata faida kubwa iliyotokana na ujuzi wake wa lugha ya mbwa na jogoo. Ilimu hiyo imempa faida na kumuokoa kutoka kwenye hasara.

Mkewe aliyekuwa akimngoja kwa hamu, baada ya kumkaribisha vizuri, alimuuliza; “Je! Farasi alifika salama sokoni na ulifanyaje?”

Tajiri alijibu kwa furaha: “Nimemuza kwa bei nzuri na nimeepuka hasara chupu chupu. Basi huyo aliyemnunua faida na hasara ni juu yake sasa na uchungu atausikia yeye, si mimi.”

Hivi ndivyo ilivyokuwa kila siku asubuhi jogoo alikikimbilia vipande vya mikate akimuacha mbwa akisononeka na kulalamika. Tajiri naye akawa atajisogeza karibu ili asikize yanayo zungumzwa na wawili hawa.


Siku ya tatu yake, Mbwa akaanza: “Ewe jogoo hivi juzi ulisema kuwa farasi wa tajiri atafariki na mzoga wake utakuwa ni riziki yangu, lakini sasa farasi ametoweka na tamaa ya mzoga uliyonipa imenitamauka.”

Jogoo aliyekuwa katika harakati za kudonadona mikate bila ya kuinua kichwa alijibu upesi upesi: “Farasi wa tajiri hivi sasa ameshafariki. Haya ninayo kwambia ni ukweli wa kuthubutu, mimi sisemi uongo. Huyu bwana alikimbilia faida chache ya darahima, hakuona uchungu kumbwagia hasara yule masikini mnunuzi. Na wewe usiwe na hofu, kaa ukijua riziki yako ni yako mwengine hawezi kukunyima ingawa ataichelewesha tu. Mwishowe itakufikia, kama si kwa mlango huu basi kwa mlango mwengine. Kama uliokosa mzoga wa farasi basi jitayarisha kwa mzoga wa punda! Kwani bwana wetu hana habari kesho jioni punda atafariki, basi jitayarisha wewe na jamaa zako kwa karamu ya nguvu hapo kesho.” Muangaza wa furaha ulionekana machoni mwa mbwa, lakini macho ya tajiri yalijawa na kiza kwa kuchelea hasara.

Mara moja tajiri aliwaza: “Sasa mimi lakufanya ni kuwahi haraka kumuza huyu punda kabla hajanifia hapa kwangu akanitia hasara. Huyu jogoo ametabiri tena jambo lisilopendeza. Pengine hii ndiyo heri ili niepukane na hasara na maafa mengine! Bila shaka huku kujuwa litakalotukia kabla halijatokea ni neema kubwa kwangu.”

Bila ya kuaga, tajiri huyo akiwa na punda, aliandamana pamoja na mtumwa wake hadi sokoni na kumuza yule punda kwa bei ya faida mno!

Kila siku asubuhi mbwa na jogoo waliendelea kusutana. Mbwa aliyekuwa na hasira siku hiyo, alibweka hadi jogoo akakereka. “Wewe ambaye ni mwenye kufahamu na kudai kuwa husemi uongo, je mzoga wa punda nao umekuwaje? Jogoo aliyekuwa ametatizika alijibu: “Hii



ndiyo mara yangu ya kwanza kuona nusu ya utabiri wangu umeghibu na kupotea mbele ya macho yangu. Lakini hata hivyo, sitaacha kukwambia mengine mapya, kwani kesho mtumwa wa tajiri ataaga dunia, na watakao kuja mazishini watapikiwa chakula ambacho wewe utafaidika nacho pia!”

Mbwa alimwalia kwa dharau na bila kuamini maneno hayo akasema: “Huo ni uongo mwengine, na utabiri wako vilevile ni uongo mtupu.”

Tajiri aliyekuwa akifurahia majibizano haya, kusikia habari ya kufa kwa mtumwa wake hakujitamalaki tena. Alishituka na kusema: “Ati, mtumwa wangu muaminifu niliyeishi naye vizuri miaka yote hii kesho atafariki dunia! Masikini alinihudumikia kwa bidii sana na kujaribu kunifurahisha kwa kila njia anayoweza. Naona kwanzia sasa hapana faida kumueka katika milki yangu!”

Tajiri aliharakisha na kuanza kupanga namna ya kwenda kumuza katika soko la watumwa. Mtumwa huyu masikini alishangazwa na hatua inayochukuliwa na tajiri wake. Alimtaradhia sana na kumtaka kwa unyenyekevu asimuuze kwa mtu mwengine, lakini bidii yake yote hiyo haikufua dafu. Alimsihi na kumuangukia miguuni na kumhakikishia kuwa ataongeza juhudi katika kazi zake, lakini wapi sikio la kufa haliskii la mteka maji msikitini, ng’o!

Tajiri kwa furaha na majivuno tele huku aliwaza na kuwazua peke yake: “Lau ni singemwambia Musa anifunze lugha za wanyama ningepata hasara kubwa sana leo. Hata hivyo ninamshukuru Mungu kwa kumfanya Musa anifunze lugha ya wanyama wawili hawa. Je! Ningeepuka vipi hizi?!”

Tajiri kwa hamu ya kutaka kujua zaidi juu ya mazungumzo ya mbwa na jogoo alisahau lengo aliloelezwa na Nabii Musa (a.s) la kutaka kujua lugha za wanyama. Alisahau malengo hayo yalikuwa ni kuboresha maisha ya hao wanyama, kuipa nguvu imani yake ya dini na kuitakasa roho yake mbele za Mwenyezi Mungu. Pato la ulimwengu dogo lilimshughulisha hadi akakosa ukinaifu. Hakuwa ni mwenye kutosheka kwa alichu nacho. Tamaa isiyokuwa na mwisho imemkalia mbele na ya akhera ameyatema.

Alifurahika na kujiambia: “Toka niifahamu lugha ya mbwa na jogoo nimepata kunusurika na hasara mara tatu sasa.

Mbwa siku ya pili kwa kejeli: “Haya, na leo unalipi lakusema kwenye utabiri wako wa uongo na kweli?”

Jogoo kwa utani: “Samahani! Eeh mbwa mpweke uliye masikini! Nimefanya kosa gani? Wakerekwa na chakula nilacho? Pengine bahati

yako ndiyo mbaya!”

Mbwa akajibu: “Tosha sasa, muongo wewe! Hila zako zimefika kikomo. Muongo nimiekusindikiza mpaka mlangoni, huna la kusema tena!”

Kwa ghadhabu Jogoo alijibu: “Mimi sisemi uongo! Hakuna jogoo anayesema uongo katu! Kwa uwezo tulionao wa Mola kila asubuhi tunawajulisha waja wakati wa swala ukiwadia. Tunapima mwendo wa jua kwa uangalifu sana na wakati hautupotei. Uongo haupo katika damu zetu asilani.” Mbwa aliyapuuza yote hayo bila kusema kitu, akajitia purukushani.

Jogoo aliendelea kusema: “Kesho tajiri atakufa ingawa ni kijana mwenye afia yake. Mrithi wake kwa kumuekea matanga atachinja ng’ombe. Basi hayo mabaki yatakayo kuepo unayoyapenda yataenea hapa. Utayaonea raha ule shibe yako.”

Ghafa tajiri kusikia maneno hayo ndipo azindukapo na kutanabahi, kuwa vifo vya farasi, punda na mtumwa, vilikuwa ni mtihani kutoka kwa Mwenyezi Mungu! Alitumia kile kipawa cha kufahamu lugha za wanyama kujitakia faida za kilimwengu. Alisahau ibada zenye kumpa faida za kiroho. Aliukatisha umri wake alipowafanyia wengine uovu alipowauzia watu mali ambayo alijua haita dumu bali itakuwa ni ya kuwatia chungu na hasara tu.

Kijana alijuta majuto ya Firauni. Mate yalimkauka akawa hana mashiko kwa hofu ya kifo iliyomjaa moyoni. Bila ya kupoteza wakati aliinuka na kuelekea nyumbani kwa Nabii Musa (a.s) na kumuelezea kisa chake haraka haraka na kumtaka ampatilize ili amuokoe.

Musa alimwambia: “Ewe kijana, sasa basi nenda ukajiuze wewe mwenyewe pia! Kwani wewe ni bingwa wa kuwasukumia wengine hasara na kuwatia machungu? Basi sasa nenda ukajiuze wewe mwenyewe vilevile kama ulivyo wauza uliowamiliki hapo mbeleni. Nilikutambua kutoka siku ya kwanza na nilikunasihi uwachane na tamaa yako hiyo, lakini kiza cha mali kilikutia upofu wa moyo ukakosa kuyaona yaliyokuwa wazi. Kila ulichokihitaji kutoka kwa Mola alikupa bila kumuomba, na ambayo hakukupa ni kwa faida na salama yako.”

“Ewe Mtume Musa kunishikilia kigogoto sio njia ya kuniokoa. Mimi nilikosea kwa ujinga wangu na sasa najuta mara elfu moja kwa yale niliyoyafanya. Sasa niombe msamaha kwa Mwenyezi Mungu anisamehe na anikubalie toba yangu” Yule kijana alilia na kusema hayo kwa Mtume Musa (a.s)

Nabii Musa (a.s) aliinua mikono yake na kumuomba kijana huyu msamaha kutoka kwa Mola wake.

“Neema zote anazokupa Mola si uhodari wako bali ni rehema zake akuinue daraja yako katika maisha ya Akhera. Uwatendee watu mema kama unavyopenda kutendewa na kuwa na uhusiano mzuri wa manufaa baina ya waja ndiko kupanda kwako” alisema Mtume Musa (a.s)

Soko la Marashi

PDF Compressor Free Version

Mkausha ngozi katika soko la wauza marashi



Wapokezi wa habari, wanukuzi wa athari na kasuku wenye maneno kama asali wameeleza kuwa hapo zama za kale, paliishi mtu mmoja ambaye shughuli yake ilikuwa ni kukausha na kushughulikia ngozi za wanyama kwa kuzitia dawa ili zisioze. Aliianza kazi hiyo tangu utotoni na akaendelea nayo mpaka ujanani mwake. Miaka mingi alikiajiriwa katika kiwanda hiki na kile cha kushughulikia ngozi. Alipata ujuzi na maarifa yasiyo kifani. Hatimaye, aliweza kufungua kiwanda chake binafsi naye angali bado kijana.

Katika habari zilizopokewa ilisemekana kuwa miongoni mwa maelfu ya wanaume wenye nguvu ambao waliifanya kazi hii,

kuna wachache wa kuhesabika walioivumilia shida na dhiki ya kazi hiyo nzito. Hivyo ndivyo hujikuza na wakawa watu stadi wenye umahiri kwenye shughuli hiyo.

Mkausha ngozi huyu naye alikuwa ni miongoni mwa watu waliohesabika kwa vidole walioweza kuvumilia dhiki na tafshani za kazi hiyo kwa roho moja, na kuendelea kubaki hadi kufikia cheo cha ukufunzi. Hakulalamika wala hakuonyesha kutoridhishwa na machovu bali aliifurahia na kuipenda kazi yake.

Kazi ya ngozi mbali na kuwa ni ngumu na yenye kuchosha pia ilikuwa ni yenye harufu mbaya yenye kuudhi wengi. Harufu hiyo mbaya ilitokana na zile dawa alizozitumia kuhifadhia ngozi ili zisiharibike. Kwa kuwa yeye alikuwa ameshaizowea harufu hiyo kutoka utotoni mwake, hisia zake zilimfisha ganzi akawa hata haimkeri wala haitambui tena. Wengi wa marafiki zake hawakuweza kuistahamia ama kuivumilia harufu hiyo mbovu. Kwa hivyo, walimtema na kumuepuka. Ahali zake waliitambua kuwa harufu hiyo iliwaudhi wengi. Hata hivyo, kazi yenyewe ilikuwa ni yenye mapato makubwa na mazuri. Yeye mwenyewe alikiwausia watoto wake kuwa “kazi mbaya si mchezo mwema.”

Siku moja kama ilivyokuwa ada yake baada ya kupata kifungua kinywa asubuhi, alijitayarisha kuelekea kiwandani kwake kushughulikia kazi yake alimuaga mkewe. Mkewe alimshindikiza mpaka mlangoni na akamwambia: “Subiri kidogo nina mazungumzo.”

Mkausha ngozi aliuliza kwa mshangao: “Mazungumzo wakati huu, huoni kuwa nachelewa na ngozi za kondoo zimepaliana kiwandani?”

Mkewe: “Tafadhali leo pitia soko la manukato ununue chupa ya uturi jioni uje nayo kwani usiku wa leo itatubidi tuende harusini.”

Mkausha ngozi akauliza kwa mshangao: “Uturi! Wataka uturi uufanyie nini?! Jee ni upepo wa ujana umekupepea kichwani?”

Mkewe alikunja sura na kuuliza bila kuchelewa: “Kwa hivyo wamaanisha mimi nimeshazeeke?!”

Bwana huyo kwa kuwa hakutaka mjadala uwe moto nyakati kama hizo, alitabasamu na kusema: “Usiyaweke moyoni, nilikuwa nakutania. Hilo lilikuwa ni swali tu! Yaani uturi wayatakiani? Na imekuwaje umetamani manukato leo?”

Mkewe alijibu kwa ukali: “Wewe zaidi ya mtu yeyote yule wajua kuwa harufu ya ngozi haipo kiwandani tu bali kila uendapo waandamania nayo na kila usiku wabebana nayo na kuileta nyumbani kwako. Sote hapa nyumbani twanuka huo uvundo wako wa dawa za ngozi!”

Bwana huyo alimtizama mkewe kwa ukali na kumuuliza: “Ati wanuka uvundo wangu wa dawa za ngozi?”

Mkewe, alirudi nyuma kwa maneno aliyoyatamka, basi aliligeuza sauti na kusema: “Usiyaweke moyoni, bwana! Lakini leo kuna harusi tungetaka angalau tujiandae vizuri kwa mavazi yakupendeza na manukato ya kunukia, tutangamane na watu tusheherekee kwa furaha na mbwembwe!”

Bwana aliyekuwa ameshaelewa nia na hali ya mkewe, alizungumza kwa ulaini na kusema: “Sawa, nitapitia madukani Mungu Akipenda, kwa wauzaji manukato nikuchagulie uturi mzuri wa kukufurahisha moyo nikuletee.”

Bwana huyo badala ya kuelekea kiwandani kwake kama kawaida yake kila siku, aligeuza njia na kuelekea soko la wauza marashi na manukato. Wakati alipoingia soko la wauza marashi, ushawishi usiokuwa wa kawaida ulimuingia rohani.

Mkausha ngozi huyo kadri alivyozidi kuingia ndani ya soko la wauza marashi hali yake ilizidi kuwa mbaya. Akiwa angali kwenye hali hii alifikia duka liliojaa chupa za marashi za aina aina, ndogo na kubwa, za miundo tofauti. Yeye hakuwa na ujuzi wowote wa kutambua daraja na ubora wa manukato. Hakujua vile atakavyochagua na kununua marashi yatakayompendeza mkewe nyumbani. Alijaribu kutembelea maduka mengine ili aweze kuwa na uchaguzi mpana, lakini alihisi kuwa miguu yake haipo chini ya hiyari yake tena. Alishikwa na kisunzi na hali ya kuchafukwa na roho, bila kujua ni nini kimetokea au ni nini kinachomdhuru.

Aliwaza na kufikiria: “Imekuwaje nimepatikana na hali kama hii, kwani nimekumbwa na nini? Sijawahipo kupatikana na hali kama hii, si utotoni wala ujanani; na nilipotoka hali yangu ilikuwa sawa na nzuri; kwani nimedhurika na nini?”

Alichukua hatua mbili tatu hivi kwa shida na juhudi nyingi, aliweza kusogea mbele kiasi. Mwili ulianza kumtetemeka na



kifua kilimbana moyo ukadhoofika. Alihisi soko inazunguka juu ya kichwa chake, alijitahidi kusogea kipembeni ili apate nguzo ajiegemeze kwayo; lakini mara moja aliishiwa na nguvu na kuanguka chini na akapotewa na fahamu. Alisikia sauti za watu kwa mbali watu waliokuwa wamemzingira kutaka kujua kwani yeye amepatikana na nini? Lakini kwa bahati nzuri hapo alipoangukia hapakuwa mbali na duka la ndugu yake aliyepewa habari ya kuzimia kwake.

Huyo bwana alifunga duka lake haraka na kuelekea makao ya wauza marashi hapo alipoangukia mkausha ngozi. Watu wengi walimzingira na kila mmoja akiwa ni mwenye kusema mawazo yake. Yeye alikwenda upande wa kichwa na kuufungua ukope wa jicho moja baada ya moja ili kukisia hali ya nduguye, alimuinua mikono na kumwita lakini hakupata majibu. Alieka sikio lake juu ya kifua cha ndugu yake ili kusikiza pigo la moyo na hapo ndipo harufu isiyopendeza ya ngozi ilipompiga na uso na fikra fulani ikamjia kichwani.

Alimwambia kijana aliyekuwa amesimama karibu hapo: “Mchunge tafadhali, mimi natoweka kidogo na hivi punde nitarudi na dawa yake upesi, usiwaruhusu watu kumkusanyikia karibu yake.”

Ndugu ya mkausha ngozi alitoka sokoni haraka na akaingia sehemu iliyokuwa imebomoka na kutelekezwa ambapo kundi la mbwa lilikuwa na mazoea ya kutembea ovyo sehemu hiyo. Haikupita mda mrefu ndipo aliporudi na mkono ameufumba. Aliketi upande wa kichwa cha nduguye na akamuomba kijana ainame ili watu wasishuhudie jinsi anavyomponya ndungu yake. Bwana huyo alifungua mkono wake na kuuweka taratibu mbele ya pua ya ndugu yake ili amnasishe dawa aliyokuwa nayo mkononi.

Bwana huyo mkausha ngozi, baada ya kupata harufu hiyo alipiga chafya mara moja na aliinuka kuketi. Alimuelezea nduguye sababu za yeye kuja upande huu ni kutaka kununua manukato yenye kunukia.

Ndugu ya mkausha ngozi alimshauri: “Kabla hali yako haijharibika tena kwa mara ya pili, afadhali upaondoke hapa palipoenea harufu za uturi mbalimbali, usije ukaanguka tena. Mimi mwenyewe nitanunua marashi mazuri na yenye kunukia

vizuri nikuletee nyumbani, kabla hamjatoka.”

Baada ya kumuokoa ndugu yake alirudi dukani kwake huku akiwaacha watu wamepigwa na mshangao na kustajabishwa na yale waliyoyaona. Walidhani kuwa huyu bwana ni lazima alikuwa ni mganga hodari, kwani wao walimshuhudia akiinama na kumsomea nduguye kitu nduguye na papo hapo akainuka!

Hii ndiyo kaida ya watu wanapo shuhudia sehemu ya jambo hulikamilisha kwa uvumi na maoni yao ya kibinafsi, ingawa ukweli uko mbali sana na wanayo yaeneza.

La kushangaza na kustajabisha ni kwamba pumba la ngozi zilizo oza ndizo alizonukishwa kwani aliyemtibu alielewa kuwa bongo lilizoea uvundo halitibiki ila kwa uvundo, na hii ndiyo siri ambayo wengi wa watu hawakuitambua.

Mshonaji Stadi na mwerevu

PDF Compressor Free Version

Wapokezi wa khabari na wanukuzi wa athari na kasuku wenye maneno ya asali wameeleza kuwa hapo zamani za kale, paliishi mshonaji mmoja mahiri. Alipata umashuhuri kwa sababu ya ufundi wake. Ushonaji wake ulikuwa umetimia kikamilifu na ukizungumzia mbinu zake na wepesi wa mkono wake ulikuwa ni maarufu.

Mshonaji tunayemueleza katika hekaya hii yetu, japokuwa alikuwa mshonaji hodari sana hakukosa ila. Watu wote walikuwa wakilijua. Tatizo alokuwa nayo ni uzoefu wa kuiba vipande vya vitambaa vya wateja wake. Hata hivyo, kwa sababu ya utalamu na umahiri wake wa ushonaji, watu bado walikuwa wakimuendea ili wampe vitambaa vyao awashonee nguo zao, wakiwa papo hapo ili wamchunge asiwaibie. Ingawaje huyu mshonaji alikuwa ni mwingi wa hila na vitimbi, wizi wake huupitisha pale anapokata kitambaa mbele ya macho ya wateja wake, kwa jinsi ambayo hata mteja anayehusika hagundui katu.

Kwa sifa hii mshonaji alijinaki na kujigamba hata mwisho akatoa biri kuwa hakuna yeyote anayeweza kumzuia asinyakue kwa vyovyote vile katika kitambaa chochote anachotewa kushona. Watu wengi waliwahi kukekana naye masharti lakini walishindwa kumnasa alipokuwa akiwaibia. Haya hufanyika peupeni nao wnatizama bila kutanabahi. Hata hivyo aliweza kuwaibia na mwisho wa kwisha alimuonesha mteja awaye kiasi cha kitambaa alichomkwapulia kiustadi.

Sifa hii ya ujanja na ustadi wake wa kuiba vitambaa vya wateja, ilienea mpaka miji ya jirani pia. Hakuna mtu aliyeweza kumgundua hila zake katika kuiba vitambaa, kwani alikuwa ni mwenye kutumia mbinu tofauti na zisizo fanana katika kuiba, hadi baadhi ya watu waliamini anawaibia kwa kiini macho.

Wapokezi wa khabari na wanukuzi wa athari wanesema kuwa yeye alikuwa anawadanganya wateja wake kila mmoja kwa mbinu tofauti na kumghafilisha kwa udhaifu wa hawaa za kila mteja.

Huyu mshonaji, kama vile msomi hodari wa nafsi na ilimu

ya uigizaji aliyetopea, alikuwa kwanza akimchunguza sura, mienendo na mazungumzo ya mteja wake kwa makini sana. Kwa namna hii alipata kuujua udhaifu wa kila mteja anayekuja kwake. Alimuundia mbinu za kuvaana na udhaifu huo bila ya khofu wala wasiwasi na kuwa mteja hatamgundua, hapo anapomkwapulia kitambaa chake.

Siku moja kijana mmoja tajiri, mwerevu na mwenye kuona mbali aliamua kumpelekea huyu mshonaji kitambaa ikiwa ni biri kwamba yeye ndiye atakayemuweza mshonaji na bila shaka atamnasa na kumshika ujanja wake.

Siku moja kijana huyu tajiri alijadiliana na wenzake mkahawani kuhusiana na umahiri na uhodari wa mshonaji huyo anayeiba vitambaa vya wateja. Katika majadiliano hayo kijana tajiri hatimaye alisema: “Mimi niko tayari kuweka changamoto kuwa huyu mshonaji hataweza kuniibia katika kitambaa change. Kwani nitachunga harakati za mikono yake kadiri ya kuwa sitomruhusu anyafue kitambaa changu hata kidogo.”

Mmoja kati ya wenziwe hapo mkahawani alisema: “Ewe rafiki, hakuna yeyote anaye shuku uwerevu na akili yako. Lakini hata hivyo hutoweza kushindana na uwerevu wa mshonaji huyo. Wewe ni kijana bado ungali mbichi, na yeye ni mzee na amebobea katika kazi yake. Yale unayoyaona kwenye kioo, yeye anayaona kwenye uso wa tofali bichi; na watu wengi waliekeana masharti kushindana kwa hilo, lakini wote walishindwa.”

Mmoja kati ya marafiki aliuliza: “Niambie nijue, sharti lako waekeana nini?”

Kijana tajiri mara moja alijibu: “Ni juu ya farasi wangu!”

Kwa kauli hiyo kimya kizito kilitawala kikao hicho ndani ya mkahawa. Wote waliokuwa hapo walikuwa wakijua kijana huyo tajiri anamiliki farasi mweupe ambae katika mbio na harakati hana kifani. Farasi anayekimbia kama upepo, na mwendo wa kifahari, kila mtu alitamani awe niwake.

Kijana baada ya mda kiasi, aliendelea: “Lau kama mshonaji huyu mwerevu ataweza kuiba kitambaa changu, basi mimi nitakubali kushindwa na nitamkabidhi farasi wangu, na lau kama mshonaji hatoweza kuiba kitambaa changu, basi mimi ndiye mshindi na nitakae mshinda naye ni lazima anipe na mimi farasi.

Na si lazima anipe farasi mwenye kusifika sawa na farasi wangu, kwa kuwa sote tunajua kuwa farasi kama huyu wangu si rahisi kupatikana. Na mshindani wangu akiwa hana farasi basi itabidi anilipe kiasi cha bei wa farasi wakawaida. Je yupo basi, aliye tayari kuekeana sharti hili?”

Kwa mara nyingine kimya kilitawala kwa muda, hakuna aliyejaribu kufungua mdomo wake ili biri kujitokeza kushiriki kwenye sharti hili. Waliokuwepo hapo hawakuwa na shaka kuwa mshonaji mwerevu ataiba kitambaa cha kijana tajiri. Kwa upande mwingine hakuna lisilowezezana huenda kijana akamshinda mshonaji huyo katika mbinu zake za kuiba. Uwezekano huu japo kuwa ulikuwa mdogo sana, uliwatia watu wengi wasiwasi na hamu. Kwa sababu hii, waliohudhuria hawakuwa na uhakika kwa litakalotokea.

Ghafla kimya hicho kilivunjwa kwa sauti ya kijana mmoja aliyekuwa na msimamo imara na yakini. Waliokuwepo hapo wote waligeuka kumtizama, wote walikuwa wanamfahamu kuwa ni kijana aliyefilisika na hana chochote katika mali ya ufahari wa kidunia. Wanajua kuwa milki yake ni mkeka nyumbani, hana mmea ardhini wala nyota angani katika mbingu saba, basi ni nguvu gani iliyomfanya akubali kushindana huku?

Kijana tajiri alimchunguza mshindani wake masikini kuanzia kichwani hadi miguuni na kwa upole alimwambia: “Nimefurahishwa na ushujaa na imani yako, lakini sote tunajua kuwa wewe huna farasi wa kunipa iwapo mimi nitakuwa mshindi, wala huna hela za kunilipa angalao bei ya farasi mmoja wakawaida!”

Kijana masikini, kwanza alimtizama kijana tajiri kisha waliokuwepo hapo na kujibu kwa sauti ya kujimakini na kujiamini: “Mimi nina yakini kuwa wewe utashindwa na mimi nitaibuka mshindi!”

Kijana tajiri aliuliza: “Ni lipi lililokufanya uwe na yakini kiasi hii?”

Kijana masikini alijibu: “Kwa kuwa najua yule mshonaji ni mwenye hila na werevu kiasi gani.”

Kijana masikini aliendelea: “Nyinyi nyote mwajua kuwa mimi sina chochote. Lakini natoa ahadi ya kiungwana kuwa nikishindwa katika hili, badala ya farasi ama bei ya farasi, nitakuwa ni mwenye kumuhudumia mwaka moja na kutii maamrishi yake bila swali

wala hoja, nitamfanyia kazi bure bila malipo yoyote!”

Kijana tajiri, aliyekuwa anajiamini kwa uwerevu na akili yake alidhani kwa yakini kuwa ataibuka mshindi. Alimtizama kijana masikini na kusema: “Sina budi ila kukubali sharti lako, kwa sababu mbali na wewe hakuna aliyejitokeza. Lakini nakunasihhi usishindane na mimi kwenye hili, kwani bila shaka kwenye shindano la sharti hili wewe ndiye utakayeshindwa. Mshonaji, na uwerevu wake wote, hatoweza kuiba kitambaa changu hata kiasi cha ukucha. Sasa basi bado ungali na nafasi ya kughairi nia yako hii!”

Kesho yake asubuhi, kijana tajiri alibeba kitambaa chake cha bei ya ghali na kuelekea kwenye duka la mshonaji. Mshonaji mwerevu aliyekuwa ni mwenye kumsubiri kuja kwake kwa hamu, kwani marafiki zake usiku walikuwa washamfikishia ujumbe wa biri waliyoekeana baina ya kijana tajiri na kijana masikini. Yeye alikuwa tayari kumuonesha huyo kijana tajiri mwenye majivuno, hali ya uwerevu na uhodari wake.

Mshonaji alikuwa ameketi akisubiri huku moyoni akisema: “Ewe kijana mbichi na wakudanganyika kirahisi, wajiona kuwa umwerevu kuliko mimi? Wataka kushindana na uibuke mshindi katika sharti hili! Lakini kuanzia hivi sasa ujihesabu kuwa umeshindwa na farasi wako amekutoka. Nitaiba vipande kadhaa vya kitambaa chako kiasi ya kuwa hata roho yako haitokuwa na habari!”

Kijana tajiri aliwasili na kumsalimia. Mshonaji mwerevu alimsifu kijana na sifa za kumtukuza na kusema: “Amani na amani tele juu yako, ewe kijana mwerevu na mwenye maumbile ya kupendeza. Umenifaharisha sana kwa binafsi kuja kwako kwa miguu yako kazini kwangu!”

Kijana, alivutiwa na tabia na heshima ya mshonaji mwerevu, alimuekea kitambaa chake mbele yake na akasema: “Ewe mshonaji hodari, kutokana na kitambaa hichi nataka unishonee joho ambalo nitaweza kulitumia pahali popote. Iwe ni kwenye sherehe ama mazishi, iwe ni katika amani ama vitani. Ishone upande wake wa juu uwe ni mwembamba na upande wa chini uwe mpana!”

Mshonaji alijipendekeza na kutabasamu akimvutia na



kumtukuzwa kwa mara nyingine kisha akasema: “Nitalishona jinsi unavyolitaka wewe. Nyembamba juu lipendeze mwili na chini pana lisishike miguu”

Mshonaji mwerevu alipata kusikia kuwa kijana huyo tajiri anapenda sana hekaya za kuchekesha, basi aliamua kuutumia udhaifu huu kiukamilifu.

Mwanzo alipima urefu wa kijana huyo na kuandika kwenye daftari. Kisha alichukua kitambaa na kuanza kukikata kwa makasi. Kijana tajiri alijiambia moyoni: “Sitaondoa macho yangu mikononi mwako hata kidogo ili nione utafanya kiini macho gani uibe kitambaa changu!”

Mshonaji mwerevu, alipokuwa akiendelea kukata, alimtizama kijana tajiri na akasema: “Muheshimiwa, ili kichwa kipate utulivu na usihisi uchovu, nikiendelea na kazi ya kukata kitambaa, nitakusimulia hekaya na kumbukumbu zilizo baki kutoka kwa wateja wakitambo. Najua kuwa wapenda hekaya za kuchekesha na mimi si mchache katika kunukuu hekaya za kuchekesha!”

Mshonaji alianza kutoa hekaya ya kwanza. Kijana tajiri, alipenda sana hekaya za kuchekesha tangu utotoni mwake, basi aliposikia hekaya hii ya kwanza, alivutiwa na namna ya utoaji hadithi wa huyo mshonaji mwerevu kiasi ya kuwa alisahau kila kitu na kuanza kucheka.

Kijana tajiri, aliyekuwa na sura nzuri alikuwa na macho madogo, ambayo wakati wakucheka macho yake yalikuwa yakifungika. Mshonaji mwerevu alipo ona kuwa macho madogo ya kijana yanafungika wakati wa kucheka, alitumia nafasi hii kukata kipande cha kitambaa na kukirusha chini ya meza yake.

Kijana tajiri alipo ona kuwa mshonaji amenyamaza na hekaya yake imefika mwisho, alisema: “Hekaya hii ilikuwa ni yenye kuchekesha kweli. Fundi umri wangu wote sijapata kusikia hekaya ya kuchekesha kama hii, ikiwezekana, nisimulie hekaya nyingine!”

Mshonaji aliwaza kiasi kisha akasema: “Sawa kabisa, hii ni kwa ajili ya kupendezwa kwako, nitakutolea hekaya ya pili. Hekaya hii ni ya kuchekesha zaidi ya hekaya ya awali. Basi itabidi unipe ahadi kuwa hutojisahau na hutozimia kwa kucheka sana!”

Kijana alianza kucheka kwa sauti, mshonaji akasema: “Mbona

wacheka hata bado sijaanza hekaya yangu?”

Kijana alisema: “Maneno yako ni ya kuchekesha sana. Hekaya wazitoa hata kabla ya mtu haja isikia yuwaanza kucheka. Ni kama vile wamtekenya msikilizaji kwa macho yako, bila kutaka mtu atacheka!”

Mshonaji alinukuu hekaya ya pili kwa umahiri kabisa. Kijana alikosa hisia za kujimiliki kwa kicheko alichocheka mpaka akaanguka chini akitaataa. Mbinu zake zote za kuidhibiti kicheko chake, hazikufaulu. Kwa mpasuko huu wa kicheko kijana hakutanabahi kabisa kuwa mshonaji mwerevu akimbwekulia kitambaa chake kipande kipande.

Kijana macho yake madogo yalitokwa na machozi kwa kucheka sana yakawa yanamtiririka, na katika hali ya kumalizia kicheko chake, alisema akikata kata maneno: “Na kweli...ilikuwa...ni... nimekaribia kupasuka matumbo kwa kucheka!”

Mshonaji mwerevu, kwa kitambo cha kusimulia hizo hekaya mbili, aliwahi kujikatia katika kitambaa hicho cha huyo kijana kilichokuwa cha bei ya ghali, vipande vilivyokuwa si haba kwa mahitaji yake. Pale anapomaliza hekaya anayoisimulia ananyamaza kwa muda, hivyo kijana anaanza kumbembeleza mshonaji “Ewe fundi mheshimiwa, nitolee kisa kingine!”

Mshonaji aliringa na kujipurukusha kwanza, kisha akaanza hekaya ya tatu. Kama kawaida kijana alianza kucheka kwa mara nyingine na akaghafilika kabisa na lengo lake la awali, pasi na kujua kuwa kila hekaya anayo isikia na kumchekesha, inamtia gharama.

Mshonaji alimaliza hekaya ya tatu akiwa ameshajikatia kitambaa kingine cha kutosha.

Kijana alimbembeleza tena na shauku kubwa zaidi: “Ewe fundi muheshimiwa mwenye maneno matamu, na kusihi na naomba unitumbuize kwa hekaya nyingine! Tafadhali usinikatalie!”

Mshonaji alichunguza kiasi ya kitambaa kilichobaki na kwa moyoni alimsikitikia kijana, akijiambia: “Ewe kijana mpumbavu, uliyefikiria kuwa wewe umwerevu mno zaidi yangu, na kuwa ulitarajia kunishika mkono nikuibiapo kitambaa chako, mpaka sasa umeruka patupu. Lau ungelijuwa ni kiasi gani ya kitambaa chako nimeshakibwekua, ungepandwa na bokhari. Lakini

sasa tosha, hata Mungu hatofurahia niendeleo na hekaya za kuchekesha zaidi ya hapa. Umepumbazika hadi ukasahau kazi iliyokuleta hapa na wala hujazinduka kwa hasara itakayo kupata. Na bado ungali wanihimiza nisumilie hekaya nyingine! Lakini kwangu mimi hapana tena haja ya hekaya nyengine, kwangu imetosha. Nimeshapora kitambaa chakutosha na nimefanikiwa na langu. Kusimulia hekaya nyingine kwangu haina tena faida, bali ni kujichosha. Bora yamalizikie papa hapa!”

Mshonaji alielekeza sura za kikazi akamtizama kijana na kumwambia bila mzaha: “Ewe kijana, hekaya tena zimetosha, kwako wewe na kwangu mimi pia. Mimi nishachoka na zaidi sikumbuki hekaya nyingine ili nikutolee!”

Kijana hakuyafahamu maneno haya alizidi kumbembeleza na kumsihi: “Niambie kisa kingine, hekaya nyingine moja tu!”

Mshonaji alisema: “Kijana, imetosha sasa, nimesema kuwa hekaya zangu zimekwisha hazina tena maana.”

Kijana alimshikilia mshonaji na kumbembeleza zaidi: “Nisimulie kisa kingine! Nakushika magoti na kidevu cha Mtume tafadhali nisimulie hekaya nyingine!”

Mshonaji alitabasamu na kusema moyoni: “Ewe kijana mjinga, ingetaka ujichekelee mwenyewe, hakuna kisa cha kuchekesha zaidi ya hiki chako.”


Kijana alizidi kumuhimiza mshonaji na mwenye kuhimizwa alikataa. Mpaka mshonaji alipokasirika na kuamua kuweka heshima na ulimi mtamu kando na moja kwa moja kumwambia kijana: “Ewe kijana mjinga, hata kama utanibembeleza mpaka kesho asubuhi, sitosema hekaya nyingine. Hekaya ya nne haina faida ndani yake; umefahamu ninayo kwambia?”

Kijana tajiri hakuelewa dhamiri ya mshonaji aliendelea kumbembeleza.

Mwishowe mshonaji alimuinulia sauti na kusema: “Tosha tosha, ewe mpumbavu nazi unaekunwa kwa mbuzi! Lau nakutolea hekaya nyingine wajua matokeo yake yatakuwaje?”

Kijana kwa mshangao aliuliza: “Matokeo gani tena! Kwani kutakuwaje?”

Mshonaji aliendelea: “Wakati huo joho lako litakuwa nyembamba sana na halitokufaa popote. Si harusini wala



matangani, wala si kwa amani wala vitani.”

Kijana tajiri mara moja alizinduka kana kwamba ameamka kutoka kwenye usingizi mzito wa maana. Alipigwa na mshangao akanyamaza kimya akiwa amezubaa. Akainamisha kichwa akiwa mawazoni kwa kiasi, akainua kichwa kumtizama mshonaji na papo hapo akaangua kicheko kikubwa. Mshonaji alishangazwa na kumuuliza: “ Ni nini cha kuchekesha? Sijasema lolote lakuchekesha, ni kipi kinacho kuchekesha?!”

Kijana alisema akicheka: “Kwa sababu hekaya ya kuchekesha zaidi ni hii uliyoisema; uliposema kuwa joho langu litakuwa nyembamba zaidi kwa hekaya ya nne!”

Mshonaji alipofahamu kuwa kijana angawa mjinga mwishowe alielewa madhumuni yake, alitingisha kichwa kimasihara pasi na kusema lolote. Lakini kijana alisema: “Mara hii sikuchekesha na hekaya yako, lakini nilijichekelea ujinga na ubichi wangu. Nilijichekelea kuwa tangu dakika ya awali nilishindwa kwa sharti langu na yule kijana masikini. Bila ya mimi kutambua kuwa

nimeshindwa. Farasi wangu mweupe na mrembo amenitoka kwa hekaya ya kwanza. Lakini hilo halina umuhimu, tajriba hii ya mimi kupoteza farasi ilinipa funzo la thamani. Hakika yule kijana masikini ni muhitaji zaidi wa farasi kuliko mimi. Mbali na hayo, ibaki kuwa ni siri baina yetu, hizo hekaya zote za kuchekesha na kufurahisha thamani yake ni kubwa zaidi ya farasi na kitambaa; ama wewe huja yataamali hayo, ewe fundi mshonaji mwerevu?”

Mshonaji alitowa vile vipande vya vitambaa alivyo viiba kutoka kitambaa cha kijana tajiri na kuviweka juu ya meza. Na hapo ndipo wote wawili walianguka kwa kucheka kwa sauti kubwa, wakiwa mara hii wote wakicheka pamoja bila ya kuchekana.

Bwana mla udongo

PDF Compressor Free Version

Wapokezi wa khabari na wanukuzi wa athari na kasuku wavunjaji sukari wenye maneno asali walieleza kuwa hapo zamani za kale paliishi bwana mmoja aliyekuwa akipenda kula udongo wa kihindi. Yeye tangu utotoni mwake alikuwa na mazoea ya kula mchanga. Alipokuwa na umri kiasi, katika siku za kusi, manyunyu ya mvua yalifanya mchanga unukie vizuri na kumvutia; harufu yenyewe ilimvutia sana hadi ikamsukuma aonje angalau kidogo na haya ndiyo maradhi yake yaliyotokana na mazoea ya kula mchanga.

Wapokezi wa khabari na wanukuzi wa athari na hata kasuku wavunjaji sukari wenye maneno ya asali walieleza kuwa bwana huyu alipofikia mwanzo wa ujana wake aliacha ada ya kula mchanga na kuanza kula udongo wa kihindi unao tumiwa na kina mama waja wazito. Aligundua kuwa udongo huu ulikuwa na ladha nzuri na harufu ya kunukia kushinda mchanga wowote mwingine. Bwana huyo kila alipopata udongo huo aliukimbilia kwa shauku na kuburudisha hamu yake kwa kuula huku akihisi raha sana.

Katika zama hizo wanawake waliutumia udongo huo kuosha nywele zao, kwa sababu ulizifanya nywele zao kuwa ndefu na laini na kunukia vizuri mbali na kuzuia nywele kukatika na kung'oka. Bwana huyu wa hekaya hii yetu alikuwa hajapata mke na alikuwa akiishi na mamake mzee. Kwa kuwa mamake bwana huyu alikuwa ameshazeeka hakuwa na haja ya kuosha nywele zake na udongo huo. Kwa hivyo huyu bwana hakuwa na kisibabu cha kununua udongo huo.

Siku moja baada ya siku nyingi alifikiwa na mgeni nyumbani kwake. Kwa kuwa hapakuwa na sukari nyumbani, mama mzee, alimtuma mwanawe kwenda dukani kununua sukari. Bwana mla udongo alikwenda upesi madukani akaingia duka la kuuza vyakula na kutaka kilo mbili za sukari. Muuzaji vyakula aliyekuwa ni mtu mwenye tamaa na hila nyingi, aliujuu udhaifu wa huyu bwana wa tabia na ada yake ya kula udongo, alimtizama na kusema: "Udongo, ndiyo mawe ya mizani yangu. Ukiwa na haja

ya sukari utainunua hivyo!”

Bwana mla udongo aliugundua ujanja wa muuza vyakula, akaanza kumdadisi huku akificha ugunduzi wake huo, aliuliza: “Kwa nini? Kwani mawe yako ya mizani yamekuaje?” Papo hapo muuza vyakula akaunda ujanja mwingine baada ya kumtizama bwana mla udongo na kujibu: “Kusema kweli, ni mda tangu mwizi mmoja aliponiibia mawe ya mizani yangu. Huyu mwizi mwenye tabia mbaya bila shaka alikuwa ni mwerevu sana ndipo akaweza kuyaiba mawe yote ya mizani yangu mbele ya macho yangu. Mimi ni mezeeka na nimekuwa na udhaifu wakuona na wa kumbukumbu, nimekuwa na sahau nyingi zaidi. Kwa hali yoyote ile nina mapande ya udongo ya kuoshea nywele yenye uzito wa kilo mbili ambayo nayatumia badala mawe ya mizani. Basi kama utakubali, hiyari ni yako, sema ili nikupimie sukari, ama sivyo waweza kununua katika duka lingine!”

Bwana mla udongo alijibu: “Kwa hakika nina haraka, kuna mgeni mpendwa amekuja nyumbani kwetu, na mama ameshaandaa chai na yuwanisubiri mimi nimpeshe sukari nyumbani upesi. Nitainunua sukari hapa dukani kwako, kipimo kiwe na kwa jiwe la mizani au udongo wa kuoshea nywele kwangu hakuna tofauti yoyote ile.”

Muuzaji aliweka pande la udongo wa kuoshea nywele kwenye kitasa cha upande mmoja wa mizani na akainama ili kutoa sukari guniani. Bwana mla udongo hamumu ya kula udongo huo ilimshika na hakuweza kuimiliki nafsi kwa hamu ya kunyafua angalau kidinya katika kipindi kile. Katika kitambo kile kifupi wakati wa muuzaji kuchota sukari guniani mla udongo aliwahi kunyafua kijipande kidogo na kukibwaka haraka sana, huku moyoni amkitaka muuzaji awe na ajizi.

Muuzaji aliyekuwa na tamaa, alijua nia ya mteja wake bwana mla udongo, alifanya ajizi kwa makusudi kutowa sukari guniani na kuchukua mda mrefu. Hata alipokuja nayo aliweka katika kitasa cha upande wa pili wa mizani na ikadhihiri kuwa uzito wa sukari ulikuwa ni zaidi ya udongo wa kitasa cha kwanza. Muuzaji ili kumpa mla udongo nafasi zaidi, aligeuka huku na kule na kusema: “Akili yangu yenda ikidhoofika; mara sikumbuki tena chombo cha kuchotea sukari nimekiweka wapi, labda nacho pia

kimeshaibiwa. Kwa uhakika zama zimebadilika tupo katika zama sampuli. Itanibidi niende chemba nirudi na chombo chengine cha kutekea sukari!”

Alipo yasikia maneno haya mla udongo – ungesema sukari imemyayukia mdomoni kwa ute kumtoka – akasema: “Hamna tatizo babangu, nenda ukatafute chombo chengine kwa utaratibu usiwe na haraka; mimi nitakusubiri!”

Muuzaji naye alikuwa moyoni anaucheka upumbavu wa mla udongo na kusema: “Hewala, nitakwenda na wewe usiwe na haraka na ule udongo kidiri uwezao kwani haya yanayojiri yana manufaa kwetu sote sisi wawili!”

Muuzaji aliinua pazia lililokuwa limegawanya sehemu ya chemba na duka, na akaingia ndani, na akawa anamchungulia kwa pembeni mwa pazia. Mla udongo alifurahia nafasi hii, na kwa shauku na pupa alinyafua kidonge cha udongo na kuula, na vidonge vyengine akivificha katika kilemba chake.

Mla udongo ingawa kwa hamu akipapia kuula udongo huo, lakini kwa tume akitizama tizama pazia na kwa haraka akibugia vipande udongo anavyovinyafua. Aliendelea namna hiyo ili muuzaji asije akamfumana kwa ghafula.

Muuzaji kwa tamaa yake, alikuwa akimchungulia kwa kipembeni kwa raha zake zote na huku akigusa gusa vitu na kutoa sauti akitoa taswira ya kuwa angali anatafuta tafuta hicho chombo ili mla udongo aendelee kula vidonge vyake vya udongo anavyo vinyafua nyafua kwa kupatiliza.

Macho ya muuzaji yaliutizama mwili wa mla udongo uliokuwa umeparara kwa athari ya kula mchanga na udongo, huku moyoni kwake aliendelea kucheka na kutoa sauti za pirika pirika kuonyesha kuwa bado hajapata anachokitafuta.

Baada ya mda kiasi muuzaji alitokea nyuma ya pazia na chombo mkononi, na kupima sukari. Wakati huo alipima sukari ikiwa uzito wa udongo umepungua kwa kiasi kikubwa mno na kumkabidhia mkononi huyo mteja wake aliyeanza kuelekea nyumbani. Muuzaji alijinong’oneza na kusema: “Nimefurahi sana, kwa sababu nimempimia sukari isiyo zidi kilo moja kwa thamani ya kilo mbili. Na la zaidi ni kuwa kuanzia hivi sasa, mteja huyu atakuwa ni wa daima hapa kwangu. Yeye anifikiria kuwa

mimi ni mpumbavu kwa kuwa ameweza kunyafua udongo wangu akijiona ana akili. Kwa ujinga wake mimi ndiye niliyefaidika!”

PDF Compressor Free Version
Wapokezi wa khabari na wanukuzi wa athari na kasuku wavunja sukari wenye maneno asali wanasema kuwa hata wao hawakuweza kujua kuwa kwenye hikaya hii, mjinga na mpumbavu wa kweli ni yupi baina ya hawa watu wawili?!

PDF Compressor Free Version

Mwigo:	sura unayoiona kwenye kioo au maji
Tenge tahanani:	kuchanganyikiwa
Kufuja:	Utumiaji mbaya
Hakumsaza:	Hakumbakisha
Alisoza:	Alikiangamiza
Amkidhie:	Amtekelezea
Alibheneka:	Alihangaika
Unyende:	Ukelele
Pulika:	Sikiza kwa makini
Alipokifu kicheko:	Alipoacha kucheka
Bawaba:	Pata ya mlango
Komeo:	Kipingwa cha mlango
ulimbwende:	Starehe ya hali ya juu
Shari wala bari:	Baya wala zuri
Maozi:	Maono
Hawakuutanganya:	Hawakuufikia mwisho wake
Hawaiji:	Viungo vya chakula
Hodhi zenye maji:	Vidimbwi vyenye maji
Amerengwa:	Ameshangazwa
Akabaki kulaitika:	Alibaki kujilaumu
Akasinyaa:	Akanyauka
Kwa mzizimo:	Kwa ubaridi
Janibu:	Upande
Mtambaji:	Mwenye kunukuu
Anamsairi:	kwa kunyenyekea
Kidazi:	Upara
Kozi:	Aina ya Mwewe

Msamiati

PDF Compressor Free Version

Mwehu:	Mwenda wazimu
Imenitamauka:	Tamaa imetoka
Ukinaifu:	Kutosheka
Ampatilize:	Amuwahi
Kunishikilia kigogoto:	Kunitajiatajia saa zote
Dhiki:	Matatizo au taabu
Tafshani:	Masumbuko
Zimeपालiana:	Zimepandana
Chupa ya uturi:	Chupa ya marashi
Biri:	Thubutu
Alichomkwapulia:	Alichomwibia

PDF Compressor Free Version

PDF Compressor Free Version

PDF Compressor Free Version



Mawlana Jalalud-din al Rumi

*'Ziguse mbingu kwa moyo wako'.
Rumi*

Jalalu Deen Rumi aliishi katika karne ya kumi na tatu miladiya. Ana umashuhuri katika fani ya utunzi wa ushairi. Alikuwa pia mwanazuoni wa kiislamu. Tunzi zake zilikuwa katika lugha ya kifarsi ambayo ilikuwa ndiyo lugha ya wasomi maeneo kati ya Uhispania hadi bara Hindi. Umashuhuri wake ndio ulipelekea kufasiriwa kwa tunzi zake katika lugha mbali mbali.

Alizaliwa mwaka wa 1207 AD eneo ambalo sasa lajulikana kama nchi ya Tajikistan, ilokuwa chini ya dola ya Uajemi. Rumi alisafiri katika dola zima la Uajemi kasha akatulia Uturuki ambako aliaga mwaka wa 1273 AD.

Mathnawi ni mkusanyiko wa kimashairi wenye mafunzo na visa vya kina. Visa hivi vimetolewa kusherehesha maudhui mbali mbali ya akhlaqi. Visa hivi ni vya hekima vyenye makusudio ya kusisitiza hisia za kindani za kisufi.

Visa vilokusanywa katika kitabu hiki ni baadhi tu ya tarjama ya maelfu ya tunzi zake. Ni simulizi ambazo zina mafunzo kwa watu wote bila kuzingatia umri, dini wala aina yoyote ya tofauti zinazotajika.